

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report of**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, YATTA**

**CONSTITUENCY, HELD AT MATUU CATHOLIC CHURCH**

**ON**

**OCTOBER 16, 2002**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, YATTA CONSTITUENCY, HELD AT MATUU  
CATHOLIC CHURCH HALL ON 16<sup>TH</sup> OCTOBER, 2002**

**Present:**

Mrs. Abida Ali Aroni

Commissioner

**Secretariat Staff In Attendance:**

1. Collins Mukewa

Programme Officer

2. Suzanne Mutile
3. Rose Kimeu

Verbatim Recorder  
District Coordinator

The meeting started at 11.00 a.m.

**Rose Kimeu:** Habari zenu? Wacha tuanze mkutano wetu wa leo kwa maombi na ningependa kumuuliza Mheshimiwa Gideon Mutiso atufungulie mkutano wetu wa leo.

**Gideon Mutiso:** Tuombe. Mungu Baba Mwenyezi, tumeinamisha vichwa vyetu hapa mbele yako, ili tukutukuze katika jambo lile ambalo liko mbele yetu. Pia, tunaomba nehema zako na wema wako utuongoze, mwangaza wako utuongoze katika akili na roho zetu, ndivyo mambo ambazo tumzungumuza, mambo ambayo tumtumini ya kwamba (inaudible) kwetu, ambaye yanahusiana na Katiba ya nchi yetu, Baba utufunulie tuweze kuona mwangaza wako. Sote tumjiweka mikononi mwako, na wale Commissioners ambao wako mbele yetu hapa, ambao watatufunulia mneno yote ambayo yako ndani ya hiyo Katiba mpya, ambayo tunataraji kwa mapenzi yako Baba, wewe unajua ni mpenzi ya watu wako wa Kenya, tuongoze na Katiba mpya, ndipo mambo yote ambayo yako mbele yetu tuweze kuyatimiliza tukifuatia muundo wa Katiba mpya. Baba, tujiweka mikononi mwako utubariki na roho wa Mtakatifu atushukie na kutufunika na uwezo wake, ili mwangaza wake uendelee nasi, kwanza katika mwanzo wa mkutano huu, hadi mwisho wake. Tunaomba hayo Baba tukiamini ya kwamba unatusikia na utatimiza. Katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amen.

**Rose Kimeu:** Asante sana Mheshimiwa Mutiso. Ningependa kuwakaribisha tena kwa mkutano wetu, na wenye mko nje ni matummaini yangu kwamba wenye wako nje mmekuja kwa mkutano ya Katiba, kwa hivyo ningewaomba muingie, nyinyi wote, tuanze na nyinyi. Wenye mko nje, tafadhali hatutaki kuona watu wamekaa nje, kama mko nasi ingieni.

Kwa matumani ya wale ni wageni, mimi kwa jina naitwa Rose Ngina Kimeu, mimi ni District Coordinator wa Constitution of Kenya Review Commission, Machakos, na wenye wamekuja na Commissioner kutoka Nairobi ni Programme Officer Collins Mukewa, Mukewa tafadhali salimia watu wa Matuu wakaweze kukuona, na Miss Mutile. Hawa ndio Programme Officers wametoka Nairobi, na kwetu sisi leo hapa Matuu, tutakuwa naye Commissioner Abida Ali Aroni, ambaye ni Commissioner mmoja wa wale wa tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya, yeye ndiye ataweza kutuongoza kwa mkutano wa leo. Singetaka kupoteza wakati mwingi ningependa kumpatia Commissioner Ali Abida Aroni nafasi akaweze kutuelezea ni yapi ama ni mambo gani ambayo yamemleta Matuu. Asanteni sana.

**Com. Ali:** Hamjambo? Ningependa kwa niamba ya Tume kuwakaribisha katika huu mkutano wa leo, na kabla hatujaanza, ningewaomba ambao mko nyuma mje mbele, ndiyo tukianza mkutano tusiwe tunaukatiza Kwasababu kuna watu wanaingia na kututazia. Tafadhali tuwache nafasi za nyumma kwa watu ambao watakuwa wanakuja tukiendelea na mkutano. Asanteni.

Ningependa kuwakaribisha tena katika mkutano huu wa leo, ambao tumetaka kuja na kukutana na nyinyi ili kuweza kuzungumzia na kuwagalia mambo ambayo yako katika pendekezo la Katiba au Draft Constitution ambayo mumeiona na ninahakika wengi wenu mumeweza kusoma kupitia makala ambazo ziliwekwa katika magazeti, karibu sasa wiki mbili zilizopita.

Kwa mkutano wa leo, programme yetu itakuwa mwanzo kabisa, ni kuwaeleza kisababu cha sisi kufika. Pili, tuwaeleze madhumuni ya urekebishaji wa Katiba, lakini nina hakika nyote mmejua ni kwanini tunarekebisha Katiba yetu kwa hivyo sitazungumzia mambo hayo, halafu tutawaeleza mambo au steps na njia tulizopitia hadi kufikia pendekezo la Katiba, halafu mwishowe tutawapa nafasi ya kuuliza maswali ikiwa kuna maswali yeyote ambayo mnayo, na pia ikiwa kuna jambo lolote ambalo mtu angependa kusema kuhusiana na hii pendekezo la Katiba.

Ningewaomba msinipatie views kwa siku ya leo, Kwasababu jambo hilo tulifika hapa na kulitekeleza. Lakini ikiwa mna mambo ambayo munataka kuyaona yameongezwa, yamepunguzwa kutoka kwenye Katiba, mnaweza kutuelezea ingawa njia bora zaidi itakuwa kuyaeleza kwa waakilishi wa District ya Machakos ambao watakuja katika kikao cha kitaifa. Mnaweza pia kuzungumza na mwakilishi wenu Bungeni, MP, kumueleza Kwasababu pia ataketi katika hicho kikao cha kitaifa. Lakini ikiwa mnataka kuyasema leo mtatueleza tuyasikie, lakini kama Tume kwa wakati huu hatuna uwezo wa kubadilisha hiyo pendekezo ila kwa kupitia katika National Conference, na hiyo National Conference kama mlivyosikia, kutakuwa na delegates mia sita ishirini na tisa. Kila District itatuma delegates watatu na hapo ndiyo kutakuwa na mjadala mkuu utakaotoa Katiba mpya ya Kenya kabla haijapitishwa Bungeni kuidhinishwa na Rais, ili iwe ni Katiba mpya ya nchi yetu.

Wakati ambapo tulifika hapa kuchukuwa maoni yenu, ninahakika mlielezwa kwamba tutarudi katika Province na sio Constituency, kuweza kufanya mjadala. Wakati ambapo tulimaliza kukusanya maoni ya wananchi mwanzo wa mwezi wa saba, Bunge likabadilisha sheria na ikawa hakuna nafasi ya kwenda katika Province Kwasababu karibu kila mtu ana haraka ya kuona kwamba tuna Katiba mpya. Tulipoweza kuandika hilo pendekezo, tukaona kwamba tuna karibu mwezi mmoja ambapo tungetumia kuja na kuzungumza na nyinyi ili kuwasiliana zaidi na mpate nafasi ya kuelewa pendekezo hilo mjitayarisha katika kikao cha kitaifa, na ndiyo namna tukakubaliana kwamba tufike katika kila Constituency na kuzungumza na watu ambao watakuwa na nafasi na pia kuwaletea rasmi pendekezo hilo la Katiba mpya.

Kwa wakati huu pendekezo ambalo mnalo ni la lugha ya Kiingereza. Kuna nakala ambazo zinatolewa kwa Kiswahili, na ninatumahi kwamba Rose atazipata hivi karibuni, Kwasababu wakati tulipotoka Nairobi wiki mbili zilizopita, tuliwacha bado zinapigwa chapa, na kwa siku ya leo hatukutoka kwa ofisi Kwasababu tulikuwa katika District ya Makueni kwa wiki moja na nusu zilizopita, na tumetoka huko na kuja hapa. Kwa hivyo, hivi karibuni mnaweza kuzipata ili msome kwa wale ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza, na kuelewa zaidi.

Sasa, baada ya kuchukua maoni yenu, tulipata watu ambao walijiriwa kuyaangalia na kuyachambua maoni hayo, Kwasababu Tume haikupata nafasi ya kuweza kufanya uchambuzi. Hapo awali kabla hatujatembea, tuliweza kuwa na warsha ama workshops na seminars tofauti ambapo tuliwasiliana na kupata mawaidha kutoka kwa wataalamu tofauti. Wataalamu ambao

wengi wao walikuwa wananchi wa Kenya ambao wamesomea mambo tofauti, waalimu wa University, ma-Professor na watu mbali mbali ambao walikuja na tukazungumza nao kuhusu mambo mbali mbali yanayo husu Katiba, pia kuna wakati ambapo tulialika wataalamu kutoka nchi za ngambo ambao tulidhania wangeweza pia kutusaidia katika mawazo yetu kwa mambo pengine ambayo yamependekezwa na yanafaa kuwangalia vile mambo hayo yameweza kuendelea katika nchi zingine.

Sasa, baada ya kuwangalia maoni yenu na tukarudia kuwangalia mambo ambayo tuliyapata katika seminars na workshop, tuliandika reporti kuhusu jinsi tulivyoelewa maoni yenu na mambo yale ambayo tuliyazungumuza. Hiyo reporti tuliweza kuichapisha katika magazeti; nafikiri sasa ni karibu wiki tatu ama mwezi tangu tulizichapisha katika toleo la magazeti hapa nchini, na pengine Bi coordinator ataweza kuwapatia nakala kidogo muweze kuangalia. Ile ambayo tumechapisha kwa wakati huu ni reporti fupi. Ile kubwa bado inafanyiwa kazi Nairobi, Kwasababu ilikuwa na kurasa nyingi zaidi na kama nilivyowaeleza tena kuna haraka ya kufanya kazi hii, lakini hilo toleo kamilifu lina maoni yote ambayo tuliyapata na pia tumeandika kwa kirefu background papers, ambazo zitawasaidia kuelewa mambo mengi ambayo yako katika pendekezo ambalo tumelitoa.

Kabla hatujaandika, tuliweza kujadiliana kwa urefu Kwasababu kuna mambo mengi ambayo tuliyasikia. Kuna yale yaliweza kuwandikwa katika Katiba, kuna yale ambayo tumependekeza yaandikwe katika sheria ambazo ziko chini ya Katiba, na kuna zingine ambazo tumependekeza ziangaliwe na serikali Kwasababu Katiba ni mwongozo, na hatuwezi kuwandika mambo yote katika Katiba. Wakati ambapo tulikuwa tunajadiliana, tulifuata utaratibu ambao umewekwa na sheria inayo tuongoza katika kazi hii, na kuna njia tatu ambazo huwa tunazitumia ili kuweza kufikia jambo lolote lile.

Mwanzo kabisa, huwa tukiwa na jambo tunashauriana, tunajadiliana, na kukubaliana kwa kauli moja, yaani kunakuwa watu wote wamekubaliana na jambo hilo. Ikiwa haikuwezekana, tunakuwa tunajadiliana kwa masaa mengi, na kujaribu kubadilishana mawazo. Hapo ikiwa watu wengi inakuwa ni wazi kwamba watu wengi wamekubaliana jambo, tunapitisha jambo hilo kwa kutumia consensus au kauli ya watu wengi, kwasababu inakuwa wazi pengine mtu mmoja au watu wawili ndio wanamafikira tofauti. Tatu, ikiwa hakuna uwazi wa sisi kukubaliana jambo, huwa tuna piga kura na watu wale ambao ni wengi basi maoni yao yanachukuliwa. Katika kuwandika Katiba hii, tulikuwa hatukukubaliana sote kwa mambo yote mara zote. Lakini, tuliweza kupata consensus, wingi wa watu, na hatukuwa na haja ya kupiga kura. Kwa hivyo, pendekezo hili la Katiba ya nchi yetu liliandikwa kupitia ushauri na kukubaliana kwa wana-Tume wengi. Nilidhania jambo hilo lilikuwa muhimu kwenu kujua, ndiyo muelewe kwamba jinsi ambavyo tulifikia kuwandika na kuweka mapendekezo ambayo mmeona katika Katiba.

Tulipokuja hapa kwenu na sehemu zingine za Kenya tukianza kuwangalia Katiba hii au pendekezo la Katiba, mlitueleza kwamba mngetaka kuona Katiba ambayo ina utangulizi. Watu wengi walilalamika wakasema kwamba Katiba ya nchi yetu haitambui wananchi. Ukiangalia, haujui kama ni Katiba ya wananchi, au ya wanyama, au ya watu gani, na mkaomba kwamba tuwe na utangulizi utakao tambua wananchi na kutambua jitihada na kazi kubwa ambayo wananchi wanafanya katika nchi yetu, na tumependekeza katika ukurasa wa pili, preamble au kwa Kiswahili utangulizi, ambao tuliweza kuwandika baada ya kuwangalia mapendekezo mengi ambayo tulipewa kutoka sehemu zote za nchi. Kwa kuanzia, utangulizi huo unaonyesha wazi

kwamba Katiba hii imeandikwa na sisi kama wananchi wa Kenya. Tumetambua wazi kwamba Katiba hii itatawala wananchi. Pia tumependekeza kwamba tutambue mambo tofauti ambayo tunayo kama wananchi wa Kenya, kwasababu sio lazima tutengane kwasababu tuna tofauti za kikabila, za kimila, za kidini, lakini tumetambua na kusema kwamba hata ingawa tuna tofauti hizo, tumeweza kuishi kwa amani na umoja kama kitu kimoja. Pia, tumeweza kutambua umuhimu wa binadamu, umuhimu wa familia na jamii katika kujenga taifa, na pia tumependekeza kwamba tutambue shughuli ambazo zimefanywa na wananchi tofauti wakati ambapo tumegombania kuwa na nchi ambayo ni ya demokrasia na inayozingatia sheria na haki za kibinadamu.

Ingawa sehemu nyingi watu walitaka tutambue watu waliopigania uhuru, pia kuna watu wengi ambao walitueleza kwamba baada ya kupata uhuru tulizidi kupigania haki za binadamu kwa njia tofauti. Kwasababu ya mambo kama hayo, tukasema hatutataja kikundi au mtu yeyote, lakini tutatambua wanawake na wanaume ambao wamepigania serikali ambayo inaweza kutambua haki, demokrasia na sheria ya nchi yetu. Hatimaye tukatambua na kumuomba Mwenyezi Mungu aweze kubariki nchi yetu. Sasa, huo ndio utangulizi. Mtauangalia muone kama ni sawa, au mngetaka kuona mabadiliko na kupendekeza zaidi ili tuwe na utangulizi pengine ambao utakuwa ni mzuri zaidi ikiwa utangulizi huu haujafaa.

Katika Chapter ya kwanza ya Katiba, tumeangalia pahali pa wananchi wa Kenya, na tukapatia wananchi wa Kenya umuhimu mkubwa zaidi na kusema kwamba mamlaka yote ya utawala huwa yako na wananchi na wananchi ndio wenye kutoa mamlaka haya kwa vyombo tofauti vya serikali. Kwa mfano, tumependekeza kwamba Bunge ambalo tumelipatia mamlaka kwa kupitia upigaji wa kura ni lazima litumie mamlaka hayo wakizingatia sheria ambazo tumeziandika katika Katiba hii. Tumependekeza kwamba pia serikali kuu ambayo tumeipatia mamlaka ya utawala ni lazima izingatie sheria kuu ya nchi yetu, na pia atakayekuwa kiongozi wa serikali, akumbuke kwamba kazi yake ni kututumikia na sio kututawala.

Tumependekeza pia kwamba tumepatia mahakama mamlaka, ili mahakama itumie mamlaka hayo kwa njia iliyo faa, kwa kuweza kutatua shida tofauti wakitumia sheria na wakitumia njia za haki na za halale. Pia, tumependekeza kuwe na mkono wa nne wa serikali ambao tunasema ni vyombo tofauti vitakavyowekwa na ki-katiba, Constitutional Offices, na tumependekeza pia chombo hicho kiweze kutumia mamlaka ambayo tutawapatia kwa njia itakayofaa na kwa njia ambayo imeandikwa katika pendekezo hili la Katiba. Pia, tumependekeza katika Article ya tatu, jinsi ambavyo tutaweza kutetea Katiba yetu na kuilinda, jambo ambalo haliko katika Katiba ya wakati huu.

Article ya nne, imeendelea pia na mazungumzo hayo, na hiyo ni tofauti kati ya Katiba tunayoipendekeza, na Katiba ambayo iko kwa wakati huu. Katika kifungo cha tano, Article tano, tumeangalia sheria zote za nchi yetu, na tukaweza kupanua sheria hizo zaidi ya vile tukonazo kwa wakati huu. Mwanzo kabisa, tumependekeza kwamba sheria kuu iwe ni Katiba. Pili tumependekeza kwamba sheria zinazotungwa na Bunge ziwe pia ni sheria za nchi yetu. Tumetambua pia sheria za mila au za kitamaduni sheria ambazo zilikuwa kwa wakati huu hazijapewa nafasi kubwa katika Katiba yetu. Jambo hili tulifanya Kwasababu sehemu nyingi tulikwenda, watu walilalamika na wakasema kwamba ingekuwa tumefuata sheria za kimilia, pengine

mambo mengi yangekuwa hayakuharibika. Kwa hivyo tumeipatia nafasi katika sheria za nchi yetu. Pia, tumependekeza kwamba jamii ya Wahindu na Waislamu wapatiwe nafasi ya kuweza pia kutumia sheria zao, kwasababu hawana sheria za kimila sheria ambazo wanatumia ni sheria za dini zao.

Pia, tumependekeza kwamba sheria zitakazotungwa na jumuiya ya Africa mashariki, ziweze kutumika hapa nchini. Hii ni Kwasababu kutakuwa hakuna haja ya kuwa tuna jumuiya ya Africa mashariki, East African Community, tumetoa pesa kule, tumetuma watu, na wakiyakubaliyana na kutunga sheria, hazitumiki hapa Kenya. Tumesema sheria zitakazotolewa na East African Community ziwe zinatumika hapa. Tumependekeza kuwa pia sheria ambazo hutokana na matumizi, common law, mambo ambayo hutumika kwa muda mwingi wakati mwingine huwa yamekuwa ni kama sheria. Korti itaweza kuwagalia na ione mambo kama hayo yatumike kutatua mambo tofauti. Wakati huu, common law ambayo tunatumia ni ya uingereza. Tunaangalia mambo ambayo yametumika sana uingereza na kutumia hapa Kenya, lakini nadhania Katiba ya wakati huu inatupa nafasi ya kutumia common law au common practice ya nchi yetu, ili kuweza kutatua shida ambazo tunazo.

Pia, tumependekeza kwamba mikataba ambayo inawekwa sahihi katika mikutano ya kitaifa ambayo inahusika na sheria mbali mbali, ikiwa Kenya itaidhinisha mikataba hiyo, iwe itaweza kutumika kama sheria. Mfano mzuri ni kwamba kwa miaka mingi tumekuwa tukiweka sahihi na kuidhinisha mikataba ya haki za binadamu, haki za watoto, haki za walemavu, haki za wakina mama, lakini tukifika Kenya tunaweka katika makabati na kusahau. Sasa tumependekeza kwamba Kenya ikiweka idhini katika mkataba wowote tukirudi hapa, mkataba huo na mambo ambao yamekubaliwa na nchi za kitaifa yatumike kama sheria ya nchi yetu.

Tukiinglia Chapter ya pili, tumeangalia na kupendekeza kwamba tutambue kwamba Kenya ni nchi ambayo ina mambo fulani, na tumependekeza mambo fulani fulani katika Chapter hiyo. Katika Article ya sita, Sub Section ya pili, tumependekeza kwamba jamhuri ya Kenya imeundwa kwa mambo au maadhili ama values and principles fulani, na tumependekeza kwamba nchi yetu itambulike kama jamhuri inayozingatia demokrasia ya vyama vingi, nchi ambayo inawahusisha wananchi wake katika utawala; nchi ambayo inatawala kwa njia ya uwazi, ya haki na inawajibika kwa wananchi wake, na nchi ambayo inazingatia tofauti za vyombo vya utawala, na pia kuzingatia haki za kibinadamu, haki za msingi na utawala wa sheria. Katika Chapter hiyo pia, tumeangalia mipaka tofauti ya Kenya na nchi jirani. Mipaka hiyo tumeiandika kwa kirefu sana katika schedule ya mwisho. Mkiangalia katika hizo nakala zenu, katika nafikiri, ukurasa wa thelathini na tisa kuendelea mbele, tumeweza kupendekeza mipaka ya Kenya na nchi jirani kwa kirefu sana. Mtaweza kusoma baadaye na kuona. Tumependekeza mipaka ya Kenya-Uganda, Kenya-Tanzania, Kenya-Sudan, Kenya-Ethiopia, mtaweza kuwaangalia na kuelewa zaidi.

Pia, tumependekeza lugha ambazo zinafaa kukuzwa na kutambuliwa. Tumependekeza kwamba Kiswahili na Kiingereza viwe ndiyo lugha rasmi. Kwa wakati huu lugha rasmi ni lugha ya Kiingereza. Ndiyo maana ukienda kortini, hata ukikaa na Judge ambaye ni mu-Afrika na ni Mkamba mwenzako, ni lazima karani afanye interpretation. Mmeona hivyo kwenye High Court? Kwasababu lugha rasmi ni lugha ya Kiingereza, na Judge anakosa kusikiza Kwasababu ameambiwa lugha ya korti ni lugha ya

Kiingereza. Sasa tunapendekeza kwamba lugha rasmi iongezewe lugha ya Kiswahili Kwasababu ni lugha ambayo inaeleweka na kutambuliwa na wananchi wote kulingana na lugha ya Kiingereza. Pia, tukapendekeza lugha ya kitaifa ibaki ikiwa ni lugha ya Kiswahili, lakini tumependekeza pia kwamba serikali ikuze lugha zote za makabila tofauti ya Kenya, ili lugha hizi ziwe zinapatiwa heshima, na zisije zikapotea ama zikadharauliwa. Pia tumependekeza kwamba serikali itambue lugha ya ishara, sign language, ambayo inatumiwa na watu walemavu, na iweze kukuza lugha hiyo pamoja na maandishi ya Braille ambayo ndiyo yanaeleweka na watu walemavu.

Tumeangalia pia ukurasa wa kumi, upande wa serikali na dini. Tumependekeza kwamba dini na serikali ziwe ni vitu tofauti, lakini hatukusema kwamba watu wa makanisa wasijihusishe na siasa. Kwa hivyo, muelewe kuna siasa na serikali. Sisi tunasema serikali iwe secular, isiwe inapendelea na kukuza dini yeyote ile. Iwe tu ni serikali inazingatia mambo yake ya kiserikali, na dini zote hapa nchini zipewe mamlaka sawa katika juhudi za kiserikali. Halafu tumependekeza vyombo ambavyo tunavipendekeza kama vyombo vya kitaifa. Vitu ambavyo tunaviita kwa Kiingereza national symbols. Tumependekeza kwa mfano, wimbo wa taifa, tumependekeza pia chapa inayatumika katika mambo mengi ya kiserikali, coat of arms, iwe ni symbol ya kitaifa. Tumependekeza pia seal, mhuri wa serikali uwe pia ni symbol ya kitaifa.

Pia tumeangalia siku za mapumziko na siku za sherehe za kitaifa, na kutoa mapendekezo kwamba tuwe na siku tatu peke yake. Kwanza tumependekeza siku ya tarehe mosi mwezi wa June, Madaraka Day itambulike kama national day. Pia tumependekeza tarehe kumi na mbili mwezi wa kumi na mbili pia itambulike, Jamhuri Day kuwa ni siku ya kitaifa. Tumependekeza pia siku nyingine ambayo ni siku itakayo tambulika kama Katiba Day. Sasa, mtaangalia muone kama hiyo ni sawa, ama kuna mambo muhimu ambayo tumewacha. Sehemu zingine tumeelezwa kwamba ni lazima tutambue Kenyatta Day au tuwe na Hero's Day, na tuondoe Katiba Day. Sasa ingekuwa vizuri hapa sehemu yenu mtupe maoni kuhusu hivyo na kupendekeza kama mnaona jambo hilo liko vipi.

Katika Chapter ya tatu, tumeangalia maadili tofauti au values and principles ambazo zitajenga nchi yetu na mambo haya tumeyafikia baada ya kuzungumza na nyinyi na watu wengine tofauti Kwasababu watu walitueleza hatuwezi kuwa na taifa lisilozingatia maadili fulani au values fulani. Hii ni Kwasababu mara kwa mara tunapata viongozi wanaokuwa na mafikira tofauti.

Hapo tumeangalia umoja wa wananchi wa Kenya na tumependekeza kwamba jambo la kwanza ambalo tunafaa kuzingatia ni umoja wa wananchi wa Kenya. Pia tumependekeza kwamba tuzingatie na kukuza tofauti zetu kwa njia inayofaa na kuzingatia democrasia itakayo tuwezesha sisi kama wananchi wa kawaida kujihusisha na shughuli za kiserikali. Tumependekeza kwamba jamhuri yetu iwe na serikali ambayo ina uwazi, na inajibika kwa wananchi wa Kenya. Tumependekeza kwamba pia serikali ijihusishe na jinsi ambavyo tutaweza kuondoa ufasidi katika nchi yetu.

Tumependekeza pia kwamba serikali iheshimu haki za kimsingi na haki za kibinadamu. Tumependekeza pia serikali itambue democrasia kupitia vyama vya kisiasa. Tumependekeza pia, tuwe na usawa bila kuwaangalia maumbile ya mtu yeyote, iwe ni jinsia yake, iwe ni kabila lake, iwe ni mtu ambaye pengine ni mlemavu. Tumependekeza pia, kuwe na jukumu muhimu kwa



serikali na kwa wazazi kwa watoto, na jinsi ambavyo watoto hawa wanalewa. Tumependekeza kwamba pia Jamhuri yetu iweze kuhakikisha kwamba rasilimali ya nchi yetu imegawanyishwa kwa njia inayofaa na kusambazwa kote nchini bila upendeleo wa aina yoyote na pia jinsi ambavyo sisi tunaweza kama Wakenya kukuza jina letu katika sehemu ya Afrika na dunia nzima. Tujitahidi na kuwa na mambo ya mandeleo ya takayo tupa sifa na nafasi katika jumuiya ya mataifa mbali mbali.

Halafu, katika Chapter hiyo ya tatu, tumeangalia ni nini majukumu ya wananchi. Mara kwa mara tunasema serikali inajukumu hili na lile, lakini hatujaangalia majukumu yetu kama wananchi, na tunapendekeza kwamba ingawa serikali ina-responsibility ya kutufanyia sisi kama wananchi na sisi tuna duties ambazo ni lazima tuzingatie kama wananchi wa Kenya. Kwanza kabisa, tumependekeza kwamba zile maadili ama golden values, haziwezi kupatikana ikiwa sisi kama wananchi wa Kenya hatukuzingatia mambo fulani. Mambo ambayo tumependekeze ni yafuatayo, kwamba ni lazima kila mwananchi ahakikishe kwamba anaelewa mambo ambayo yako katika Katiba yetu. Baada ya kuelewa mambo hayo, iwe ni jukumu letu kama wananchi kuweza kusimama imara na kuitetea Katiba ya nchi.

Pili, iwe sisi tuna jukumu kama wananchi kupiga kura wakati wa kura, na pia kuwa na jukumu la kuweza kusimama ikiwa mtu anataka kusimama na kupigiwa kura. Nne, kwamba sisi kama wananchi tuna jukumu la kufanya kazi ili kuweza kukuza familia zetu, jamii zetu, ili nchi nzima iweze kukuwa katika uchumi Kwasababu ukikosa kufanya kazi na kukuza jamii yako, uchumi wa nchi unazidi kuharibika. Pia, tukapendekeza kwamba ni haki na ni jukumu la kila mwananchi kujiendeleza kimasomo na kujipatia elimu mbali mbali ambazo zitatusaidia katika shughuli zetu, za kujenga taifa. Masomo kwa mfano, yatatusaidia katika kazi zetu, na juhudi zetu mbali mbali. Pia, tukapendekeza kwamba iwe ni jukumu la kila Mkenya kuweza kuchangia katika community yake au jamii yake ili tuweze sote kuishi kwa njia inayofaa, na kwamba iwe ni jukumu letu kama wananchi kuzingatia umoja na kukuza umoja kwa njia ya amani.

Pia, iwe ni jukumu letu kuweza kukuza democrasia na utawala wa kisheria, na pia kuhakikisha kwamba mali ya umma inachungwa na kutumiwa kwa njia inayofaa. Pia, tuweze kama wananchi kuchunga mazingara yetu tuhakikishe kwamba mito na sehemu mbali mbali, milima, mbuga na vitu kama hizo ambazo ni rasilimali zetu zinahifadhiwa. Pia, tumependekeza kwamba ni jukumu letu kama wananchi kuhakikisha kwamba tunaondoa rushwa. Hii ni Kwasababu tukisema serikali ni corrupt, ni nani huwa ana-corrupt serikali? Nani huwa anahonga? Si ni wewe? Ukipatiakana na hatia, unahonga Police asikupeleke Police Station. Si uwache akupeleke ushtakiwe, halafu na usihonge Magistrate tuone nini itakuwa. Pengine wote watakosa kuwa ni watu wenye tabia mbovu na kuweza kufanya uhaki, Kwasababu tutakuwa tumeamua kama wananchi hatutahonga mtu yeyote. Pia, tumependekeza kwamba kama tunataka jamhuri yetu ipate nafasi ambayo ina sifa nzuri katika nchi zingine iwe ni jukumu lako kama mwananchi kuhakikisha jambo hilo linafanyika na pia iwe ni jukumu letu kuhakikisha kwamba kuna usawa wa kila mwananchi katika nchi hii yetu. Sasa, nimewasomea kwa kirefu majukumu yetu kama wananchi Kwasababu nadhania jambo hilo ni muhimu sana.

Katika Chapter ya nne, tumeangalia uraia na tukapendekeza jinsi tatu ambazo mtu anaweza kupata uraia. Tukasema hivi,

kwanza kabisa, mtoto ambaye anazaliwa na mzazi yeyote, awe ni wa kike ama wa kiume ambaye ni Mkenya, atakuwa anapata uraia wa Kenya. Hapo mnaona kutakuwa na tofauti na sheria ya hapo mbeleni ambapo kulikuwa ni lazima baba awe Mkenya. Sasa tumependekeza hata mama akiwa ni Mkenya, basi mtoto yule aweze kupewa haki ya uraia. Tumependekeza pia, kwamba kuwe na watu ambao wataweza kujiandikisha ikiwa wanataka kuomba uraia wa Kenya kwa kupitia masharti ambayo yataandikwa na Bunge. Tumependekeza pia, watu ambao wameishi Kenya zaidi ya miaka saba na wakaweza kufuata masharti yatakayowekwa Bunge pia wapewe nafasi wakitaka kuwa raia wa Kenya. Tumependekeza pia kwamba, mtoto ambaye ana chini ya miaka minne na amepatikanaa humu nchini na hawezi kujitambua wazazi wake ni nani ama yeye ni Mkenya, aweze kupewa uraia wa Kenya, ili tuweze kutatua pengine shida hizi tunazo za watoto ambao wako katika mabarabara.

Tumependekeza pia, kwamba wananchi wa Kenya waweze kupata uraia zaidi ya moja. Kwa wakati huu ni hatia kwa Mkenya kuwa na uraia wa nchi nyingine. Tume angalia mapendekezo tuliyopata tumeangalia mambo yanayofanyika katika nchi zingine, tumeangalia na kutambua kwamba kuna Wakenya wengi ambao wamekwenda kutafuta maisha nchi zengine ambapo pengine ukiwa raia wa nchi hiyo, kwa mfano ukiwa raia wa Amerika unapaka manufaa mengi. Kwa hivyo, itakuwa ni kosa kumwambia Mkenya ukienda America usiwe citizen na ukiwa citizen wa huko, usiwe citizen wa Kenya. Kwa hivyo tumependekeza Mkenya apewe nafasi ya kuchukuwa uraia wa nchi nyingine akipenda. Tumependekeza pia kwamba Bunge iteue Board au kamati itakayoweza kuchunguza applications au maombi yote yatakayotumwa na watu wanaotaka kuwa raia wa Kenya, wachunguze kabla watu hawa hawajaweza kukubaliwa.

Chapter ya tano na ni muhimu, tumeangalia haki za kimsingi au haki za kibimdamu, haki ambazo tunasema hazijatolewa kwa binadamu na mtu yeyote, tunazaliwa na kupewa haki hizi na Mungu, na ni lazima zizingatiwe na kukuzwa na kupewa watu wote.

Tumependekeza kwamba haki hizi ni za kila mmoja, na ni lazima serikali ihakikishe kwamba kila mmoja ana hizo haki. Tumependekeza kwamba haki hizo zitumike ila wakati ambapo Katiba imependekeza au sheria imependekeza kwamba haki hiyo ipunguzwe. Hiyo ni Kwasababu pia haki ikiwa haina kikomo, kuna watu ambao wataitumia kwa njia mbaya, na tumeangalia kwa mfano, mara kwa mara tunasema kuna haki ya kuabudu, lakini kuna watu ambao pengine watakuja katika sehemu au vikau ambavyo watu wanaishi na kuabudu kwa kupiga kelele usiku mzima na kuingilia haki za wenzao ambao pengine ni wadini ingine na hawawezi kulala Kwasababu mtu fulani anapiga ngoma usiku mzima. Sasa tumsema, kuna haki ukipewa ya dini, lakini lazima ipunguzwe uambiwe ukiabudu, kumbuka kuna mwenzako ambaye anaabudu kivingine. Pia, tukatoa majukumu kwa serikali na kupendekeza kwamba wafanye mambo haya ili kuhakikisha kila mwananchi ana haki ambayo ni ya kimsingi. Kwa mfano, tumependekeza kwamba serikali ni lazima izingatie na iweze kukuza na kuheshimu haki ambazo ni za kimsingi. Serikali ni lazima katika mielekeo au miongozo ya kiserikali ihakikishe kwamba wamezingatia haki hizi, pia sheria zitakazotungwa ziwe zinahakikisha hazikutunyanganya haki ambazo ni za kimsingi, pia kwamba kutawekwa na Tume ya usimamizi wa haki za kimsingi kwa kupitia Bunge.

Tukiangalia baadhi ya haki ambazo tumependekeza ni haki ya maisha. Tumependekeza kwamba kila Mkenya apewe haki ya maisha na hapo kwa vile tumependekeza haki ya maisha pia tumependekeza kufutiliwa mbali kwa hukumu ya kifo. Hii ni

Kwasababu huwezi kuwa na haki ya maisha, na huku unamzuia mtu kuishi kwa kumpatia hukumu ya kifo. Tumependekeza pia, kwamba tuwe na haki ya kutokuonewa. Freedom from discrimination, na kwamba mtu yeyote asionewe na serikali na asitendewe mambo kinyume cha haki yake Kwasababu ya kabila lake, Kwasababu ya rangi yake, Kwasababu ya maumbile yake, Kwasababu ya mambo ambayo, kwa mfano, status, kama ameo, hakuoa, ni mzee, asibaguliwe hata Kwasababu ya mila au lugha au jinsi alivyozaliwa.

Tukatazama katika kifungo cha thelathini na tano, haki za akina mama. Tulifanya hivi Kwasababu akina mama walipendekeza kwamba haki zao zisipote ngwa na kuwekwa katika kifungu peke yake, basi hizo haki huwa hazitambuliki, na wakasema Katiba ya wakati huu, imewezesha wakanyanyashwa kwa miaka arobanne. Sasa wakaomba tuandike kifungu na kama mjuavyo kuna wamama wengi sasa Kenya walipozungunza, ikatubidi ni lazima tuitikie mwito wao. Tumependekeza baada ya kuwasikiza akina mama kwamba akina mama wapewe usawa pamoja na wanaume, iwe ni usawa wa kibiashara, usawa wa kisiasa na usawa katika shughuli za kijamii. Political, economic and social activities. Pia, tukapendekeza kwamba akina mama waweze kupewa haki sawa na wanaume katika umiliki wa ardhi, katika kupata nafasi za kuwawezesha wafikie mali hiyo, na pia katika uridhi wa mali.

Practice za kimila ambazo zitakosa kuwapatia akina mama heshima na kuwapatia haki zao basi sheria hiyo na mienendo hiyo ipigwe marufuku, na isemekane kwamba haiambatani na sheria za nchi hii. Pia tukapendekeza kwamba, serikali iwe na jukumu la kuwaangalia akina mama maslahi yao kwa kutambua sehemu yao muhimu ya uzazi katika nchi yetu na iwapatie nafasi ya kuweza kujikua na kuendesha shughuli zao kwa njia iliofaa. Tukaangalia pia haki za wakongwe au haki za wazee, Kwasababu wazee pia walilalamika na wakasema Katiba ya wakati huu haikuwatambua na kuweza kuwachunga. Tulipendekeza kwamba iwe ni jukumu la serikali na familia ya mtu ambaye ni mzee kuweza kumpatia usaidizi wa kutosha. Tukapendekeza pia kwamba watu hawa wazima wawe na nafasi ya kujishughulisha na mambo ya kitaifa. Wasionewe na wasinyimwe nafasi ya kuweza kufanya jambo lolote lile ambalo lingefaa kwa watu hawa.

Article 37, tukaangalia haki za watoto na haki hizi tumependekeza ya kwamba watoto ni watu ambao ni muhimu katika jamii yoyote ile, na iwe ni jukumu kwanza la wazazi, pili jukumu la familia, tatu jukumu la jamii kuwalinda, kuwalea, kuwasomesha na kuhakikisha kwamba watoto wamekuwa ni watu watakaoweza kuwa na manufaa katika jamii kwa siku zijazo. Pia, wapewe mazingara ya kufaa, wapewe mapenzi, wapewe furaha na watu wajaribu kuwaelewa wakati ambapo tunalea watoto hawa. Tumependekeza pia kwamba mtoto atakayezaliwa ndani ya ndoa au nje ya ndoa wapewe haki ya usawa ya kisheria bila kubaguliwa, na kwamba ikiwa kuna jambo lolote ambalo linatatuliwa kuhusiana na mtoto tuzingatie kwanza maslahi ya yule mtoto bila kufikiria maslahi ya baba na mama kwanza. We look at the interest of the child first, and then consider other things after that. Tumependekeza pia kwamba mama na baba wawe na jukumu sawa la kulea na kumchunga mtoto. Iwe wameoana ama hawakuoana. Pia tumependekeza kwamba kila mtoto aweze kupata jina la familia na aweze kupata uraia. Ndiyo mkaona tukasema ikiwa kuna mtoto wa miaka minane amepatikana na wazazi wake hawajulikani Kwasababu hatutaki kuwatupa na ni vigumu kujua nationality ya huyo mtoto, basi wote watoto hawa wapewe uraia wa Kenya wakipatikana nchini.

Pia tumependekeza kwamba kila mtoto aweze kupata elimu ya msingi ya bure na ya lazima, na watoto pia wachungwe dhidi ya mambo ambayo yatawadhuru. Kwa mfano, mambo ya kimila ambayo yanaweza kudhuru watoto. Pia wasinyanyaswe wala kutukanwa. Tumependekeza pia wasiweze kufanyishwa kazi ambazo zinaweza kuwapatia mambo yasiyofaa. Tumependekeza pia kwamba watoto wasipatiwe adhabu itakayoweza kuwaumiza na maadhabu ambazo hazizingatii haki za kibinadamu, iwe ni katika shule ama sehemu zozote za kutoa elimu. Pia wakati wa vita, watoto wasitumike kutumiwa katika vita, na wakishikwa, wasiwewe katika cell ambayo iko na watu wazima. Pia mtoto asifungiwe, ila ikiwa imelazimika Kwasababu ni kwa faida na manufaa ya huyo mtoto kufungiwa. Akifungiwa ni lazima serikali impatie wakili atakayeweza kumtetea kwa haraka iwezekanavyo ili aweze kutoka katika gereza. Pia, tulipendekeza kwamba mtu ambaye anajulikana kama mtoto ni ambaye ana miaka kumi na minane na kuendelea chini.

Article 38, tumependekeza kuhusu familia na kupendekeza kwamba mtu yeyote atakayekuwa amefikisha umri wa miaka kumi na minane ana haki ya kuoia ama kuolewa kwa mapenzi yake mwenyewe bila kulazimishwa, na kwamba ukisha kuingia katika ndoa, kuwe na usawa katika ndoa hiyo kwa watu ambao wameoana ndani ya ndoa, na wakati ambapo wanataka kuachana, na kwamba Bunge litahakikisha limetengeza sheria ambazo zitahakikisha jambo hilo la usawa. Pia, tumependekeza kutolewe sheria itakayo tambua ndoa ambazo zinafanywa kupitia mila tofauti. Tumetambua pia haki za watu walemavu, na tumependekeza kwamba serikali ifanye mambo yote ambayo yatawawezesha watu walemavu kupata elimu zinazofaa. Kuwapatia vifaa vitakavyo weza kuwapa elimu na pia kukuza lugha zao za ishara na kuweza kuhakikisha kwamba wanaweza kupata nafasi ya kuingia katika magari ambayo yanatumika kwa umma, public transport, na pia kuweza kuingia katika sehemu ambazo kuna mashirika ya kiserikali. Pia, kwamba sheria itatolewa ya kuhakikisha kwamba watu hawa hawakunyanyaswa na watahusishwa katika sehemu zote za utawala hapa nchini.

Tumeangalia na kupendekeza kwamba Mkenya yeyote asilazimishwe kufanya kazi ya kitumwa. Tumependekeza pia haki ya kuabudu, na tukapendekeza kwamba kila mtu awe na haki na uhuru wa kuabudu, kuwa na mafikira ya kidini, na pia kuwa na mawazo yeyote ya kidini, bila kusema ni mawazo ya aina gani. Pia, kwamba watu hawa waweze kuabudu wakiwa kama ni jamii ama ukiwa ni mtu binafsi, na vikundi vya kidini vipewe nafasi ya kuwanzisha shule na kuziangalia. Pia, Mkenya yeyote asilazimishwe kuabudu dini asiyoitaka, wala kuweza kufanya jambo lolote kinyume cha dini yake. Tumependekeza kwamba kila Mkenya aweze kupata habari zinazotolewa na serikali. Tumependekeza pia kila Mkenya aweze kuwasilisha na kujiunga na wenzake bila pingamizi, na pia tuwe na haki ya maandamano ambayo sio maandamano ya fujo.

Tumependekeza pia, haki za kisiasa, na kupendekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya kujiunga na chama chote cha kisiasa, au kuunda chama cha kisiasa ikiwa anataka kufanya vile na pia kufanya campaign ya chama chake cha kisiasa bila kuingiliwa. Pia tuwe na haki ya kupiga kura kila wakati wa kura utakapofika. Tumependekeza pia tuweze kuandikishwa kupiga kura kila wakati, na tumependekeza kuwe na haki ya kutembea na kuishi pahali popote hapa nchini. Tumependekeza haki ya wafanyi biashara na wafanyi kazi wote, na pia wapewe nafasi ya kuweza kufanya shughuli hizi, na ziwe ni shughuli halali

zinazotambulika. Tumependekeza pia haki ya kuwa na mali. Tumependekeza haki za walioajiriwa, labour relations, na tunapendekeza kwamba wafanyakazi wote waweze kupewa kazi ambazo ni za haki. Waweze kulipwa mishahara inayofaa kulingana na kazi zao, waweze pia kupatiwa wakati unaofaa wa kufanya kazi, reasonable working conditions, pia wapewe mazingara yanayofaa ya kufanyia kazi na wawe na uhuru wa kujiunga na chama chochote cha wafanyakazi, na pia wawe na uhuru wa mgomo.

Tunapendekeza pia, waajiri wawe na haki zao, kwa mfano, haki ya kujiunga na vyama vya waajiri. Tumependekeza pia social security au serikali iweze kulinda mtu yeyote ambaye hajiwezi, na hawezi kuhudumia familia yake kwa kumpatia yeye na familia yake usaidizi unaofaa. Tumependekeza kwamba kila Mkenya aweze pia kupata haki ya matibabu yanayofaa, na asinyimwe matibabu wakati wa hali ya hatari, ama anapokuwa na dharura. Ukienda kwa hospitali usifukuzwe, Kwasababu hauna mapeni. Tukapendekeza pia kuwe na haki ya elimu kwa kila Mkenya. Haki ya shule ya msingi, shule ya nursery mpaka shule ya secondari, na kwamba serikali itaweka mpango wa kuwezesha kila mtoto apate haki ya elimu ya bure ya kimsingi na pia iwezeshe kuweka mipango itakayo wezesha wananchi kusoma katika shule za upili na kujiendeleza katika institutions zingine juu ya secondary education. Pia tukaangalia makao na tukapendekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya makao yanayofaa. Mtu asitolewe katika nyumba anayoishi wala kubomolewa bila ya jambo hili kupitiwa na korti itakayo chunguza jambo hili na kutoa amri inayofaa.

Pia tukapendekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya kutokuwa na njaa, na kwamba kila Mkenya aweze kupata chakula cha kutosha na maji ambayo ni ya kutosha na safi, na kuishi katika mazingara masafi na yanayofaa. Pia tukapendekeza haki za ununuzi na tumependekeza kwamba mtu atakaye nunua huduma ama kitu chochote apewe vitu ambavyo ni sawa. Quality service and quality goods, na vitu hivyo utakavyonunua visiwe vitakudhuru afya yako ama kukuweka katika hali ya hatari au iwe ni vitu au huduma ambayo haiambatani na pesa ambazo umetoa. Tumependekeza kwamba pia tuwe na uhuru wa kukataa kutii amri ambazo si za kisheria. Tumependekeza pia tuweze kupewa nafasi ya kufikia korti bila pingamizi, ili tuweze kusuluhisha mambo yote ambayo yana mzozo. Tumetoa haki za watu watakao kuwa wameshikwa, Kwasababu watu waliteta na kusema wanatendewa mambo yasiyofaa, wakati ambapo wanashikwa. Tumependekeza kwamba mtu atakayekuwa ameshikwa awe na haki ya kunyamaza. Excuse me, can you do the distribution afterwards, because I do not expect people to listen as you are doing other things. Thank you.

Kwamba ukishikwa, uwe na haki ya kukaa kimia, bila kulazimishwa kuandika statement ama kusema chochote na kwamba ikiwa umeshikwa uambiwe kwamba ukizungumza mambo hayo yanaweza kutumiwa ili kukuhukumu na kwa hivyo ukikiri kosa lako, iwe umekiri Kwasababu umetaka mwenyewe na hukulazimishwa kuaandika confession; na kwamba utafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo na isipitishwe masaa arubaini na nane, na ukifikishwa mbele ya mahakama mara moja uelezwe kisababu cha mashtaka yako. Pia, upewe nafasi ya kutosha ya kuweza ya kujiandaa kujitetea katika mahakama. Tukapendekeza pia haki za wafungwa. Tumependekeza kwamba mtu yeyote ambaye ni mfungwa asifanyiwe mambo ambayo ni ya madhara. Aweze kupewa haki zinazostahili binadamu (interruption inaudible).

Tafadhali ningewaomba hizo nakala mzichukue baada ya programme ama mchague programme na sisi tufunge mizigo yetu tuelekee Nairobi, because we can not have an unruly meeting. Tafadhali, watu ambao mko nje mrudi ndani ama tuwawaache mkisoma twende Nairobi. You can make a choice. The person distributing, please can you stop distributing. Let us have a meeting that is orderly tafadhali. Thank you.

Chapter ya sita tumeangalia uwakilishaji Bungeni, na tukaangalia haki ambazo ni zetu katika kuwachagua watu watakao kwenda kutuwakilisha Bungeni. Kwanza kabisa tumeangalia hali ya upigaji wa kura, na tumependekeza kwamba kura ziwe ni za siri, ziwe za haki na za halali. Kura hizo pia zikipigwa tuhakikishe kwamba watu walemavu, watu ambao wametengwa, jamii ambazo zimetengwa, na akina mama wamepewa haki ya kuweza kujihusisha na kupiga kura. Tumependekeza kwamba kura ziwe za haki, na kwamba kuwandikishwa kwa upigaji kura kuendeleo kila pahali, na tumependekeza kwamba watu ambao wataweza kujiandikisha kura, kwa mfano, mtu yeyote ambaye amefikisha miaka kumi na minane, mtu yeyote ambaye kawaida anaishi katika jamhuri ya Kenya, na pia mtu ambaye hajashtakiwa na kosa lolote la kuhusika na upiganaji wa kura.

Tumependekeza kuwekwe au kuwe na mabadiliko katika Tume ya upigaji kura, Electoral Commission, na kupendekeza kwamba Tume hii ambayo ina watu ishirini na wawili ipunguzwe ili tuwe na watu nane. Wakizidi zaidi, wawe ni watu kumi. Kwasababu wananchi walilalamika na kusema kwamba kuna watu wengi zaidi. Pia, tukaangalia kwamba kuna nchi zingine zina Electoral Commission ya member mmoja lakini tukaona katika nchi yetu tungependelea kuwe na watu kutoka sehemu tofauti na tukaangalia tukasema ikiwa kuna province nane, basi tuwe na uwakilishaji wa province, na ikiwa kuna watu ambao pengine ni wazidi waongezwe wawili, wawe ni watu kumi. Tukaangalia pia shughuli na kazi ambazo zinafanywa na Electoral Commission, na tumependekeza kwamba kazi yao muhimu iwe ni uandikishaji wa wapiga kura. Wawe wanatazama sehemu za uwakilishaji Bungeni, wawe wanasimamia upigaji kura, wawe wanahakikisha kwamba kura ni za haki, na zimepigwa kwa njia ya usawa. Wawe pia wanasimamia vyama vya kisiasa, uandikishaji wa vyama vya kisiasa na kuvifutulia mbali. Wawe wanasimamia pesa ambazo tumependekeza zitengwe kwa vyama vya kisiasa. Pia wawe wanasomesha wananchi kuhusu elimu ya upigaji kura, na kuwapatia mambo zaidi kuhusu demokrasia. Pia, hiyo Tume iwe ni Tume ambayo ni huru, isiyo tangamana na siasa za pande zozote.

Tukaeleze pia, kuhusu jinsi ambavyo uwakilishaji Bungeni, mipaka yake itakavyo tengezwa, na tukapendekeza kwamba, kila baada ya miaka kumi, Tume hili liangalie hiyo mipaka au kwa Kiingereza, Constituencies, na ifanye mabadiliko ikiwa imezungumza na wananchi na imezingatia mambo ya fuatayo. Baada ya kuzungumza na wananchi, iangalie wingi wa watu katika constituency. Pia iangalie hali ya mawasiliano, iangalie hali ya geographia, iangalie matakwa ya watu wanao ishi pale, iangalie mipaka ya administration, na mwisho kabisa, iangalie census ambayo itakuwa imefanyiwa kabla ya wakati huo. Kwa kuwagalia vyama vya kisiasa, tumependekeza kwamba hata ingawa kuna haki ya kuwandikisha vyama vya kisiasa, kwamba vyama hivi vya kisiasa ni lazima viwe vina wanachama wanataokuwa wametoka sehemu zote za Kenya, isiwe ni chama cha kikabila, cha kidini ama kinachozingatia mambo ambayo si ya kitaifa, na kwamba watakusanya na kuweza kuwaletea wananchi



mambo fulani fulani ambayo yatatutasaidia katika kukuza mambo yetu ya kiuchumi. Kwamba wataweza kuhusisha wananchi kwa mambo ya kisiasa. Wataweza pia kuhakikisha kwamba serikali imewajibika kwa shughuli ambazo zimepewa kupitia katika Parliament.

Tukaeleza kwa kirefu, vyama ambavyo vinafaa kuwandikishwa na wakati gani vyama hivi vinafaa kufutuliwa mbali. Kwa mfano, tumependekeza kwamba chama ambacho kitafaa kuwandikishwa ni kile ambacho kitakuza umoja na utafu. Chama ambacho kinazingatia demokrasia na pia, kinafanya uchaguzi mara kwa mara na kinawahusisha watu wote katika jamii, iwe ni watu walemavu, akina mama, wazee na vijana. Pia chama ambacho kinaonesha wazi katika malengo yake, kwamba kitakuza Katiba na sheria ya nchi yetu. Lakini, tukapendekeza kwamba ikiwa kuna vyama ambavyo vimeundwa kwa mambo kwa mfano, ya kikabila, ya rangi, ya dini na mambo kama hayo, chama hicho kifutuliwe mbali. Chama ambacho kinajihusisha na vita na mambo yasiyofaa kifutuliwe mbali. Chama ambacho kimejiwekea jeshi ama vikundi vya vijana, para- military militia, kifutuliwa mbali. Kwa wakati huu tunasikia kuna vyama ambavyo, ama wanasiasa ambao wana vikundi vyao vya vijana ambao wanakuwa ni kama wanatoa huduma za kiserikali. Vyama kama hivyo vifutuliwe mbali. Vyama ambavyo vitaweza kutoweka vitabu vya hesabu, na kutoweza kutoa vitabu hivyo kwa mkaguzi mkuu wa serikali, pia vifutuliwa mbali.

Tumependekeza, mtaona katika Chapter ya ishirini, kwamba vyama vyote vya kisiasa tumependekeza vipewe mwaka mmoja, miezi kumi na miwili kuweza kuzingatia mambo hayo na vikikosa kuzingatia, vyama hivyo vifutuliwa mbali. Kama nilivyo waeleza, tumependekeza kwamba kutengwe pesa kadha na serikali ili kusaidia vyama vya kisiasa. Tumependekeza kwamba asilimia nukta tatu ya budget ya nchi yetu, au point three percent of the National Budget itengwe kila mwaka, ili kuhudumia vyama vya kisiasa. Tumependekeza kwamba pesa hizi zigawanywe kwa njia mbili. Sio kila chama cha kisiasa kinachoundwa kipewe pesa, lakini tunapendekeza kwamba vyama vya kisiasa vitakavyoweza kupata kura asilimia tano ya kura zote ambazo zitapigwa nchini, five percent of the total votes cast, ndiyo vipewe usaidizi. Asilimia hamsini ya pesa zitakazotengwa zigawanyishwe kwa usawa kwa vyama ambavyo vitakuwa vimeweza kupata kura zaidi ya five percent, halafu zitakazobakia, asilimia hamsini zigawanyishwe kutegemea na number ya kura ambazo kila chama kilipata.

Je, pesa hizi zitumike kwa njia gani? Tumependekeza kwamba pesa hizi zitumike kwa mfano, katika campaign na katika shughuli mbali mbali ya vyama hivi vya kisiasa, lakini pesa hizo zisitolewe kama zawadi au mishahara, na asilimia kumi peke yake ndiyo itumike katika shughuli za kuendesha ofisi tofauti ya vyama vya kisiasa. Pia, tukapendekeza kwamba vyama vya kisiasa vinaweza kupata pesa zingine kupitia kwa kujiandikisha au pesa zitakazotolewa na wanachama, au pesa zitakazotolewa kama donations na supporters wa vyama hivyo.

Chapter ya saba, tumependekeza kuhusu Bunge. Tumependekeza kwamba kuwe na vyumba viwili vya Bunge. Tumependekeza chumba ambacho tumekiita National Council, na kingine tumekiita National Assembly. Kwa njia nyingine unaweza kusema tumependekeza Upper House and Lower House. Katika Article 102, tumependekeza kazi zitakazofanywa na Bunge. Kwa mfano, kutengeza sheria za nchi, kuweza kutatua shida tofauti za nchi, kuhakikisha kwamba makadirio ya

fedha za umma zinatumiwa kwa njia inayofaa, na pia kuhakikisha kwamba Katiba hii inazingatiwa. Kuhakikisha na kuwalia mikataba tofauti ya kitaifa. Kuangalia watu wanaoingia katika baraza la mawaziri, na pia kuwalia watu wanaoteuliwa mbali mbali. Kwa mfano, watu watakaokuwa na vyeo katika serikali, pia kuwalia mienendo ya Rais, makamu wa Rais, Prime Minister au waziri mkuu, na baraza la mawaziri. Pia kuangalia hali ya hatari wakati ambapo wataona kuna hali ya hatari, na muhimu sana kuzingatia Katiba hii na kukuza demokrasia na utawala ulio bora.

Sasa, tumependekeza kwamba katika hiyo National Council au Upper House, tuwe na wanachama mia moja, ambao watachaguliwa kutoka kila district. Tumetambua kwamba tuna district sabini, na kwamba kila district iweze kuchagua mtu atakayeingia katika hiyo National Council na utaona kwamba tutakuwa na washiriki sabini. Tumependekeza kwamba viti thelathini vilivyobakia vitengwe na kupewa akina mama, na akina mama hawa tumependekeza wasitoke katika district, lakini watoke katika province na kwamba Kwasababu viti thelathini havingetosha district, tunapendekeza kwamba kila province ila Nairobi itoe wamama wanne watakao pigiwa kura, na Nairobi tukapendekeza iwe na viti viwili, na kwamba hawa watu watakaokuwa katika National Council watafanya kazi yao kwa miaka minne.

Katika National Assembly, tumependekeza kwamba tupige kura kupitia constituency kama kawaida, na hapo tutakuwa na viti mia tatu. Lakini, tukipiga kura kama kawaida kupitia constituency, tutakuwa tuna waakilishi mia mbili na kumi. Tumependekeza kwamba tutumia njia nyingine ile itakayotupatia viti vingine tisaini, kwa kutumia list intakayotolewa na vyama vya kisiasa ambavyo vina uwaakilishi Bungeni. List hii itategemea uwezo au nguvu ambayo itakuwa na kila chama, na kwamba vyama hivi katika list hiyo watakatwa watatoa kulingana na watu ambao wangetaka wewewe priority. List hiyo ikiwa mtu wa kwanza ni mwanamke wa pili awe ni mwanamme mpaka wafikie mwisho. Pia, wazingatia watu walemavu, vijana na jamii ambazo zimetengwa. Tumependekeza pia watu ambao wanaweza kuingia kwa Bunge. Tumesema kwanza ni lazima wawe ni wa-Kenya, wafikishe miaka thelathini na tano na zaidi wakitaka kuingia katika National Council. Wakitaka kuingia kwenye National Assembly wawe na miaka ishirini na moja kuendelea. Awe ni mtu ambaye anaweza kupiga kura, na amefika kiwango cha Form four, ame fika kidato cha nne, na ni mtu ambaye anaweza kuwasiliana kwa Kiswahili na Kiingereza. Kwa watu ambao ni walemavu wawe ni watu ambao wanaweza kuwasiliana kwa lugha ya ishara. Pia, wawe ni watu ambao wataweza kufuata maagizo ya ki-katiba kuhusu tabia na mienendo ya viongozi ambayo tutapitia katika schedule baadaye. Bunge hili la pili litafanya kazi yake kwa miaka mitano.

Tumependekeza kwamba, Wabunge waweze kufanya kazi zao kulingana na Katiba hii mpaka wakati ambapo Bunge litakapovunjwa, lakini tumependekeza kwamba wananchi waweze kurudisha nyumbani Wabunge ambao hawastahili kuwa kwa Bunge. Tumependekeza vitu vitatu vitakavyoweza kumuwachisha Mbunge kazi. Kwanza tumependekeza kwamba Mbunge akiwa ni mgonjwa na ana madhara ya bongo na hawezi kufanya kazi yake kwa njia inayoistahili, aweze kuwachishwa kazi. Mbunge ambaye ana tabia ya kuzozanisha na kuweka chuki baina ya watu aweze kurudishwa nyumbani, na Mbunge ambaye amekimbia eneo lake la uwaakilishi na haonekani bila kisababu cha kutosha, aweze pia kurudishwa nyumbani. Tulipendekeza njia iwe ni kwa asilimia thelathini ya wapiga kura. 30% of registered voters waweze kupendekeza petition kwa Speaker wa



Bunge. Naye Speaker wa Bunge, baada ya siku saba ya kupata malalamiko hayo ataomba Tume ya uandikishaji Bungeni kufanya mapelelezo na kuona kama malalamiko hayo ni ya ukweli. Ikiwa ni ya uoga yatatupiliwa mbali, na ikiwa ni ya ukweli, basi Speaker ataweza kutangaza kwamba kiti hicho cha Bunge kiwazi, na kuitisha election nyingine.

Sasa, mtazidi kusoma. Kuna mambo mengi kuhusu hivyo vyumba vya Parliament. Jambo ambalo pengine ningeligusia ni kwamba tumesema Parliament iwe na calendar yake, na isiweze kuvunjwa ila kufikia miaka minne kwa Upper House, na miaka mitano kwa National Assembly. Tumependekeza kwamba quorum ya nyumba, chumba chochote kile, kiwe ni aslimia thelathini ya watu au wanachama wa jumba hilo, na kwamba lugha itakayotumika Bunge ni Kiswahili, Kiingereza na lugha ya ishara. Tumependekeza pia, Bunge ziweke kamati zinazostahili kuwasaidia katika kazi yake. Tumependekeza pia, Bunge liwe na haki ya kuweza kupitisha kura ya kutokuwa na imani na waziri mkuu, ili waziri mkuu aweze kuondoka katika mamlaka. Pia tumependekeza kwamba Bunge itafanya kazi zake kwa njia ya uwazi, ili mwananchi wa kawaida aweze kujua mambo ambayo yanafanyika katika Bunge.

Tukiangalia serikali kuu, the Executive, katika Chapter ya nane, tumependekeza kwamba serikali kuu itumie mamlaka hayo kwa manufaa ya wananchi wa Kenya kwa kuzingatia sheria na kanuni za Katiba. Tumependekeza kwamba National Executive, serikali kuu iwe na watu wafuatao. Iwe na President, makamu wake na baraza la mawaziri. Tumependekeza pia mambo kadha, ambayo yanamhusu Rais, na tumependekeza mambo yafuatayo. Kwamba Rais alazimike kufanya mambo yafuatayo. Kulinda uhuru wa taifa letu, aheshimu wingi wa kitaifa, na alinde haki za kibinadamu. Tumependekeza pia alinde na atete Katiba na kanuni za sheria. Pia, amepewa jukumu muhimu ambalo ni kuidhinisha miswada au bills zote ambazo zitakuwa ni sheria kwa kupitia Bunge, na amepewa nafasi tatu za kuweza kuidhinisha bills ama sheria zinazotungwa na Parliament. Kwanza akilietewa anaweza kuweka sahihi bila kuuliza jambo lolote. Pili, ikiwa kuna uzito anaweza kurudisha Parliament na kuwaambia wasuluhishe ama wafanye jambo fulani. Tatu, anaweza kuomba ushauri wa Supreme Court ambayo tumependekeza, ili kuweza kuona kama jambo hilo linazingatia kanuni za sheria, na pia zinazingatia Katiba yetu.

Rais pia amepewa jukumu la kuhutubia Bunge. Analazimika mara moja kwa mwaka kuhutubia Bunge, lakini akipenda anaweza kuhutubia Bunge zaidi ya mara moja. Pia anaweza yeye mwenyewe kwa kupitia baraza la mawaziri, kupendekeza hatua fulani za kisheria. Rais pia anatakikana mara kwa mara kuelezewa na waziri mkuu, shughuli ambazo zimezingatiwa na serikali. Hii ni kwasababu tunapendekeza kwamba Rais asiwe mkuu wa shughuli za serikali. Kwa hivyo waziri mkuu ambaye tunapendekeza ndiyo awe mkuu wa serikali atakuwa na jukumu la kumuelezea Rais kuhusu mambo hayo mara kwa mara. Rais amepewa jukumu zifuatazo. Awe ni mkuu wa Majeshi, na awe anasimamia baraza la usalama wa kitaifa, National Security Council. Pia kupita Bunge, amepewa jukumu la kutangaza hali ya hatari au hali ya vita. Ataweza kwa kupitia kwa Tume ya huduma za mahakama kuteua ma Judge, na pia ana uwezo wa kupitia katika hilo Tume ya kuwanzisha utaratibu wa kuonda Judge yeyote katika kazi, wakati ambapo kuna malalamishi kuhusu Judge, pia ana uwezo wa kuwapokea mabalozi, na pia kuteua mabalozi wa Kenya katika nchi zingine. Kutoa misamaha rasmi, pardon of mercy, na pia kutoa tuzo tofauti za kiserikali. Pia kuongoza kwa kufungwa kwa Bunge. Lakini, akiongoza kufunga Bunge ni lazima atumie masharti ambayo yamewekwa katika Katiba.

Naye tuna makamu wa Rais. Tumependekeza kwamba huyu makamu wa Rais awe ni msaidizi wa Rais. Pia wakati atakapo chaguliwa, awe ni mtu ambaye atakuwa ni running mate, au Rais atakaye simama, atueleze haki na atuonyeshe huyu ndiye ninataka awe ni makamu wangu. Ukimpigia Rais kura akishinda, yule mwenzake atakuwa automatically ndiye Vice President. Mtu huyu ni lazima awe ni mtu atakaye weza kupewa kura angesimama kutaka kura ya u-Rais. Yaani, qualification yake ifanane na ile ya Rais, Kwasababu kuna wakati ambapo Rais hayuko na atashika kiti cha u-Rais. Pia Rais akifariki au akiwa ni mgonjwa, anaweza kupata hayo madaraka. Kwa hivyo, ni mtu anaye qualifications sawa na Rais.

Bunge nayo pia imepewa nafasi ya kuweza kupendekeza kwa kuondolewa kwa Rais, impeachment of the President, kupitia katika Supreme Court. Ikiwa asilimi sitini na tano ya wa-Bunge wataweza kuweka sahihi katika motion au mapendekezo kusema kwamba Rais huyu amefanya mambo yasiyostahili Rais, basi Speaker atapendekeza kwa Chief Justice ama mkuu wa mahakama na Supreme Court itasikiza kesi ya kumuondoa Rais mamlakani. Rais naye tumependekeza aweze kufanya kazi kwa miaka mitano na akiwa ataongezwa mamlaka, isipitishwe miaka kumi.

.....na makamu wa Rais iangaliwe na Tume itakayokuwa imepewa jukumu ya kuwangalia mapato ya watumishi wa serikali. Tumependekeza pia, kuwe na waziri mkuu. Tumependekeza kwamba baada ya siku saba baada ya Bunge kuwanza kazi zake, Rais apewe jukumu la kupendekeza kwa Speaker wa Lower House au National Assembly, jina la mtu ambaye atakuwa ni kiongozi wa chama kinacho watu wengi katika Bunge kupewa wadhifa wa kuwa waziri mkuu. Akipendekeza mtu kutoka chama kilicho na watu wengi au muungano wa vyama vingi, basi Parliament itatakiwa kuidhinisha mtu huyo ama kumkubali. Wakikataa basi sasa nafasi hiyo itapewa mkuu wa vyama vya upinzani, ili kuweza kupendekeza jina na pia ni lazima Bunge kupitisha na kuidhinisha mtu huyu ambaye amependekezwa na Leader of the Opposition. Ikiwa Bunge litakata mtu huyo, basi sasa Speaker atarudi kwa Rais na kumuomba achague katika watu wale ambao wako katika National Assembly. Si lazima awe ni mkubwa wa chama hiki ama awe ni nani, lakini mtu yeyote katika National Assembly, na mtu huyo akikubalika, basi tutaweza kuwa na waziri mkuu. Waziri mkuu tunapendekeza kwamba ashikilie ofisi yake hadi wakati ambapo atafariki, atajiuzulu, au atafutwa kazi wakati ambapo Bunge litaweza ku- tokuwa na imani na yeye.

Sasa huyu Prime Minister, atakuwa anapewa uwezo ufuatao. Atakuwa ndiye mkuu wa baraza la mawaziri, na yeye ndiye atakaye pendekeza majina kwa Bunge ya watu ambao wateuliwe kama mawaziri na wasaidizi wa mawaziri. Tumependekeza kwamba tusiwe na mawaziri watako zidi kumi na watano na wasaidizi wao, au Deputy Ministers wasizidi kuwa ni zaidi ya kumi na tano. Pia, yeye ndiye atakayekuwa anasimamia maneno ya serikali siku kwa siku. Yeye ndiye ni lazima atahudhuria Bunge kwa niaba ya serikali, na yeye ndiye atakaye simamia matumizi na makadirio ya fedha za umma. Pia ile Tume ambayo tulisema itaangalia mishahara ya Rais na makamu wake pia itaangalia mishahara ya waziri mkuu, ma-waziri na wasaidizi wa mawaziri.

Katika Chapter ya tisa, tumeangalia mahakama na shughuli za sheria hapa nchini. Katika mahakama tumependekeza kwamba mahakama ikae ilivyo, lakini tuwe na Supreme Court ambayo itakuwa ndiyo korti kuu hapa nchini. Mishahra pia ya ma-Judge

iweze kuwangaliwa na hiyo Tume itakayoangalia mishahara ya viongozi wengine. Tumependekeza kwamba hii Supreme Court, kazi yake muhimu iwe ni kutoa advice ama ushauri kwa Rais atakapowauliza. Iangalie kesi za uchaguzi wa Rais. Iangalie mambo ambayo yatahusikana na kumuondoa Rais katika kazi yake. Iangalie malalamiko yote ya ki-katiba na ikiwa kuna matatizo katika viwango tofauti vya serikali, korti hi kuu itazame mambo hayo. Mahakama yote madogo yatazingatia uamuzi wa korti hii ambayo ni Supreme Court, na tumependekeza iwe na Judge kumi ambao ni ma-Judge watateuliwa upya wasiwe ni katika ma-Judge ambao wamehudumu kwa wakati huu. Tukapendekeza pia, kwamba ma-Judge kwa wakati huu wafanye kazi hadi kufikia umri wa miaka sitini na tano, na wastaafu kwa lazima lakini Judge akfikisha miaka sitini, anaweza kustaafu akitaka. Kwa wakati huu, Judge wanafanya kazi hadi kufikia miaka sabini na miwili lakini kupitia maagizo ya wananchi ikasemekana wakati mwingine mtu akifikia umri huo, huwa hata ile wisdom inapungua. Kwa hivyo tupunguze miaka na kufika katika umri wa miaka sitini na tano. Pia tulitoa watu ambao wanaweza kuwa ni ma-Judge, qualifications of Judges, na tukapendekeza pia Judicial Service Commission ama Tume itakayo toa huduma ya mahakama. Tuliwapatia nguvu zaidi kuliko ile waliyonayo sasa, na kuwapatia kazi zaidi ambayo wanayo. Kwa mfano, wao ndio wataweza kupendekeza kwa Rais watu watakao teuliwa kama ma-Judge. Wanaweza kuwangalia hali ya kazi ya wafanyikazi wa mahakama, mara kwa mara. Wataweza pia kutoa disipline kwa watu ambao wanafanya kazi katika mahakama, na ikiwa kuna mwananchi yeyote ambaye amelalamika kuhusu mtumishi wa mahakama, wataweza kufanya upelelezi ili kuweza kutatua jambo hilo.

Halafu tumeangalia ofisi ya Attorney General na kupendekeza kwamba ofisi hii igawanishwe mara mbili. Kwamba kuwe na Attorney General ambaye atakuwa ni advisor ama anayetoa ushauri kwa serikali, na asisimamie shughuli zote za utetezi ama kesi za umma. Tulipendekeza yeye ajitenge na shughuli hizo, na kuwekwe mtu atakaye itwa Director of Public Prosecution atakaye simamia kazi ya makesi ambayo yanapendekezwa kupitia serikali. Tumependekeza pia tuwe na Public Defender au mtetezi wa haki za binadamu, ama kwa lugha nyingine, Ombudsman. Pia, tukaangalia hali na kazi ambazo zinafanywa na mawakili Kwasababu watu wengi walilalamika kuhusu mawakili. Tulipendekeza kwamba mawakili wawe na jukumu la ki-katiba la kutetea Katiba ya nchi yetu, na kwamba waweze kuheshimu na kukuza haki za kimsingi. Wakati ambapo wanafanya kazi zao, ni lazima wawe waaminifu kwa sheria za Kenya, na waaminifu kwa wateja wao. Pia wakati wanakuwa katika mahakama, wawatete wateja wao bila uwoga na mapendeleo. Pia, waweze kusaidia korti vilivyo, haja tuu wasiweze kuwa wanaharibu na kutoa siri za wateja wao.

Chapter ya kumi, tunaangalia utawala wa nchi. Tumependekeza kwamba utawala wa nchi uwe una muelekeo ufuatao. Uweze kuwapa utawala wananchi, uweze kukuza umoja wa wananchi na kuzingatia tofauti tulizonazo, uweze kuhakikisha kwamba kuna democrasia na pia uwajibikishaji na uwazi katika shughuli za kutekeleza utawala huo. Kwamba utawala pia ukuze hali ya kijamii na hali ya kiuchumi, kuweze kutafutwa njia ambayo itaweza kugawanyisha rasilimali za nchi yetu kwa njia ya haki na ya usawa, na pia kuweza kukuza haki za watu ambao wametengwa katika jamii na pia kukuza uhusiano tofauti wa vyeo tofauti vya utawala. Tulipendekeza kwamba katika utawala, ni lazima one third iwe imetengwa na kuhusishwa akina mama. Tulipendekeza utawala, ufwatao. Tuwe na utawala wa vijiji, utawala wa kata ama location, utawala wa wilaya na utawala wa mkoa.

Tukapendekeza kwamba provincial administration iondelewe, kwa hivyo tukapendekeza Chief, Assistant Chief, DO, DC na PC waondolewe na serikali iweze kuwapatia kazi katika sehemu zingine ila katika utawala. Tumependekeza kwamba katika utawala wa vijiji, wapatiwe nafasi wazee wa vijiji waweze kuwa ndio wasimamizi, ni ikiwa haiwezekani katika kijiji chochote kuwa na wazee kama wasimamizi kufanywe kura ya kuchagua wasimamizi. Na kwamba, watawala hawa wawe ni watu sita, wakizidi sana wasizidi kumi. Wahusishe wananchi ili kuwangali njia iliyo bora katika utawala wa kijiji hicho. Halafu katika utawala wa kata ama location, tumependekeza kwamba locations zote au vijiji vyote vya location hiyo vitoe watu wawili watakaokaa katika utawala huo wa location, na kwamba watu hawa wawili ni lazima mmoja awe ni mama. Kwa hivyo kila kijiji katika location kitatumma either mama na mzee, au wakipenda wamama wawili Kwasababu sheria imesema lazima wamama wawe kule, lakini haijapendekeza wazee. Tuna-assume kwamba lazima wazee watakuwa pale. Wao pia waweze kuchagua msimamizi wa shughuli zao.

Halafu, tumependekeza District, utawala wa District na kupendekeza kwamba kwamba District ndiyo iwe na nguvu zaidi katika utawala wa serikali, na kupendekeza kwamba District iwe na watu watakao chaguliwa kwa kupitia kura, Kwasababu mamlaka yote yako pale. Kwa hivyo, watu wote watakao taka kusimama na kuwa katika utawala wa District itabidi wapigiwe kura kama tunavyopiga kura kawaida. Pia msimaizi ama administrator itambidi pia apigiwe kura na wananchi. Mkiangalia katika schedule upande wa nyuma, tumeeleza kazi zitakazofanywa na watawala wa District. Wao ndio watasimamia fedha zote zitakazokuwa zinakusanywa katika District. Wataangalia hali ya mabarabara, hali za huduma tofauti, mashule, hospitali na mambo kama hayo. Wataangalia masoko, na pia kuona jinsi ambavyo rasilimali itagawanyishwa.

Halafu, tumependekeza utawala wa mkoa. Ingawa tumesema utawala mwingi utakuwa katika District, tumewapatia kazi ambayo watafanya. Tumependekeza kwamba katika mkoa kila District ipendekeze majina mawili ambayo yatakuwa katika utawala wa mkoa na kazi yao itakuwa ni kuwasaidia wale ambao wako katika District ili kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kutosha wa kufanya kazi yao ya District; ya kuwatengenezea plan na policies ambazo zitatumika katika District ambapo kutakuwa na shughuli nyingi. Ikiwa kuna institutions ambazo ni za province, basi wataweza kuziangalia na kuzitumikia.

Chapter ya kumi na moja, tunazungumzia kuhusu mashamba na mali. Tumependekeza kwamba mara kwa mara serikali itatoa misimamo na mielekeo itakayohakikisha kwamba kuna usawa katika kupata mali na huduma tofauti ambazo zinatokana au utajiri unaotokana na shamba. Kwamba serikali itahakikisha kwamba mashamba yanatumika kwa njia inayofaa, na njia ambayo inaweza kuwa ni ya manufaa, Tulitambua kwamba kuna aina tofauti za sheria zinazokabidhi mashamba. Tulipendekeza kwamba kuwekwe Tume ya kusimamia hali ya mashamba ili kuweza kuwaangalia sheria hizi tofauti, na kuhakikisha kwamba sheria hizi hazigongani na zinaambatana. Watakuwa ndio wasimamizi wa mali yote ya umma, na wataweza pia kutatua matatizo tofauti tuliyoambiwa na wananchi kufikia miaka miwili baada ya Katiba hii kuwanzishwa rasmi.

Chapter ya kumi na mbili, tunaangalia mazingara na mali rasmi ya nchi yetu. Tulipendekeza juhudi za serikali na zetu kama

wananchi katika kuchunga rasilimali na mazingara ya nchi yetu na tukapendekeza kuteuliwe kamati itakayo shughulikia shughuli za mazingara.

Chapter ya kumi na tatu, tunaangalia fedha za umma na jini ambavyo zinatumiwa. Tumependekeza kwamba Bunge lisimamie shughuli ya fedha za umma, na pesa zitakazo tengwa katika juhudi za kiserikali. Tumependekeza pia kabla serikali haijachukuwa mkopo nchini ama nchi za ngambo, mambo haya yashughulikiwe na Parliament. Tumependekeza pia kwamba ile ofisi ya Controller and Auditor General igawanyishwe mara mbili, ili tuweze kuwa na huduma inayofaa. Tumependekeza tuwe na Controller of Budget, mtu atakaye simamia makadirio ya fedha, na kuhakikisha fedha hizo zinakwenda na kutumiwa kwa njia iliyostahili. Auditor General na yeye awe ni mkaguzi, Kwasababu huwezi kusimamia fedha na uwe ni mkaguzi mwenyewe. Sasa tumependekeza mkaguzi awe ni mtu tofauti. Tumetoa pia mapendekezo kuhusu Banki Kuu ya nchi yetu, na pia kutambua kwamba ofisi ya Governor wa Banki Kuu ni ofisi ya ki-katiba, na tumependekeza kwamba mtu huyu anafanye kazi ile, isizidishwe maika mitano. Pia, tukapendekeza kazi zitakazokuwa zinafanywa na Bank Kuu

Tumeangalia huduma ya umma, Public Service katika Chapter ya kumi na nne, na tukapendekeza maadili au values ambazo zingezingatiwa na watu wanaotumikia umma. Tukapendekeza mambo yafuatayo. Kwamba watu hawa ni lazima wawe na nidhamu na kuwa wanafanya kazi yao kwa hali inayostahili na ya juu, na watakapo kuwa wanafanya shughuli hizi, ni lazima wafanye kwa njia ambayo inastahili ili isiwe inaharibu uchumi wetu. Wawe ni watu wanaotenda haki. Wawe ni watu ambao watatutumikia kwa haraka iwezekanavyo. Wawe ni watu watakao fanya kazi zao kwa uwazi, na watakapo teuliwa na kupewa madaraka, wapewe Kwasababu wanastahili kwa kazi yao nzuri. Wakati ambapo wanapewa training, iwe training hii inapewa bila kupendelea kabila la mtu au mtu huyu ni mama ama mtu huyu ni hivi na vile. Pia, wakati ambapo wanaandikwa, serikali ihakikishe kwamba watu hawa wanatoka katika sehemu zote za nchi yetu. Pia, tukapendekeza kuwe na Tume ya huduma ya umma, Public Service Commission, na tukawapatia kazi ambazo pengine mtasoma baadaye na kuona kama zinafaa. Pia katika huduma, tuliangalia huduma ya usalama na tukaona kwamba huduma ya usalama inafaa kuzingatiwa katika katiba, kwasababu kwa wakati huu Katiba yetu haijazungumza chochote kuhusu huduma za usalama. Tuliangalia huduma zinazotolewa na ma-Polisi, Polisi wa utawala, Wanajeshi ambao ni Majeshi ya Ulinzi, Majeshi ya Wanamaji na pia Kikosi cha Upelelezi, na tukapendekeza values, au maadili ambayo vikosi hizi zinafaa kuzingatia katika huduma zake. Tumependekeza kwamba huduma hizi za usalama zisijiunge na siasa za pande zozote. Ziwe na udhabiti kwa raia. Pia zihesimu demokrasia, kanuni za sheria na haki za kibinadamu, ziwe na uwazi na ziajibike kwa wananchi wa Kenya. Ziongozwe na sheria katika kati zake.

Pia kwa upande wa Majeshi, tunapendekeza kwamba wasitii amri yeyote kinyume cha sheria. Pia tunapendekeza kwamba vikosi hivi vyote vijihusishe na vitendo vitakavyo tuletewa manufaa katika uchumi wa nchi yetu. Vilinde uhuru wa nchi yetu, na vilinde wananchi wakati ambapo kuna dharura ama kunashida, na wafanye kazi yao kwa uzalendo na nidhamu ya hali ya juu. Jambo ambalo ningetaka pia kusema ni kwamba tunapendekeza kwamba huduma la magereza libadilishwe jina. Kwa wakati huu tunaiita Kenya Prisons, na sisi tunapendekeza liitwe Kenya Correctional Services, ili kuweza pengine kubadilisha tabia za watu ambao wanafanya kazi huko, Kwasababu watu wanopelekwa kule katika magereza, wanapelekwa ili wasaidiwe kugeuza

tabia na mienendo yao, ili wakirudi katika jamii wawe ni watu ambao wanaweza kukaa na kuishughulisha na kazi inayostahili. Pia tukapendekeza wakati ambapo tulikuwa tunabadilisha jina, kwamba watu ambao wanafanya kazi katika huduma hizi za jela wawe ni watu ambao wanazingatia haki za kibinadamu kwa hali ya juu, wakati ambapo wanahudumia wafungwa. Pia wakumbuke kwamba wazingatie haki ambazo ni haki za kufanya binadamu astahili kuwa ni binadamu, na wajiepushe na hongo na mambo mengine ambayo hayastahili.

Katika Chapter ya kumi na tano, tumeangalia kamati itakayo simamia usalama wa nchi. Katika Chapter ya kumi na sita, tumeangalia mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa na viongozi. Katika Chapter ya kumi na saba, tumeangalia vyombo ambavyo tumesema ni vyombo vya ki-katiba. Tumependekeza vyombo fulani ambavyo tunapendekeza viwe vinasaidia serikali katika huduma na utawala kwa wananchi. Tumependekeza kwamba tuwe na Tume ya huduma ya umma ambayo ni Public Service Commission, itakayo angalia shughuli zinazofanywa na watu wanao tumikia katika mashirika tofauti ya serikali. Tumependekeza huduma ya mahakama, Judicial Service Commission, kama nilivyowaambia, huduma ya Bunge, Parliamentary Service Commission.

Pia, tumependekeza Tume ya haki za kibinadamu ni kiutawala. Kwa Kiingereza Human Rights and Administrative of Justice Commission, ambayo itaangalia mambo yanayo husika na haki za kibinadamu. Tumependekeza pia, tume ya maadili na uaminifu, The Ethics and Integrity Commission. Tumependekeza Tume ya uchaguzi kama nilivyowaambia. Tumependekeza Tume ya mishahara na malipo kama nilivyowaambia, tumependekeza Tume ya Katiba, tumependekeza pia, mkuu wa sheria, ofisi yake iwe ni ofisi ya Katiba. Tumependekeza pia wakili wa umma au Public Defender, ofisi yake iwe ni ofisi ya Katiba. Governor wa Banki Kuu, na pia Controller of Budget iwe ni ofisi ya kikatiba. Auditor General iwe ni ofisi ya kikatiba, na pia tuwe na Tume ya Ardhi, na kwamba hivi vyombo vyote vizingatie mambo ambayo yako katika Katiba.

Katika Chapter ya kumi na nane, tumependekeza jinsi ambavyo Katiba ya nchi yetu itakavyo badilishwa, na tumependekeza kwamba two thirds majority, au asilimia sitini na tano iweze kubadilisha Katiba yetu, ila kwa sehemu ambazo tumezitoa. Kwa mfano, tumependekeza kwamba sehemu za Katiba ambazo zinahusika na mamlaka ya wananchi, zinazohusika na maadili tunayofuata, zinazohusika na haki za kimsingi na pia zinazohusika na uraia, na pia hii Chapter ya kumi na nane, hizo zisibadilishwe na Bunge. Ikiwa kuna haja ya kufanya mabadiliko, wananchi wahusishwe kupitia kura ya maoni, lakini sehemu zote zingine ziweze kubadilishwa na Bunge.

Chapter ya kumi na tisa, tumeangalia maana ya maneno tofauti ambayo yametumika. Chapter ya ishirini, tumeangalia mambo tutakayo takiwa kuyafanya ili kupitia kutoka kwa Katiba mzee hadi Katiba mpya. Halafu, tumekuja katika schedule ambazo niliwaeleza. Ya kwanza tunaangalia mipaka tofauti ya nchi yetu na majirani kwa kirefu sana. Ukiangalia schedule ya pili, tumeangalia wilaya na mikoa tofauti ya nchi yetu. Schedule ya tatu tumeangalia national symbols au vyombo vya kitaifa. Bendera ya Kenya, wimbo wa taifa, alama rasmi ya serikali na muhuri rasmi wa serikali. Schedule ya nne tumeangalia viapo tofauti vitakavyo tumiwa na wakubwa au viongozi. Schedule ya tano tumeangalia mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa na watu



wote na viongozi wote wanao jihusisha na kazi za umma. Schedule ya sita tumeangalia mambo yanayostahili kufanywa na Bunge, ili kuhakikisha kwamba Katiba yetu imekamili. Tuklipatia muda kazi hizi Kwasababu kuna zile haiwezi kufanyika kwa mara moja, na kuna pia zile ni lazima zifanywe mara kwa mara bila kupatiwa muda wa kuvikamilisha. Schedule ya saba na ya mwisho, tumeangalia nguvu na mamlaka ya serikali ya wilaya na serikali kuu. Samahani, schedule ya nane tumeangalia kwa kirefu mambo muhimu ambayo yatatekelezwa wakati huu, hadi kufikia Katiba mpya.

Tumeangalia haki na majukumu ya kiserikali, tumeangalia sheria ambazo ziko kwa wakati huu na pengine hazitakubaliana kwa maneno yake na Katiba mpya. Tumeangalia upigaji wa kura na kusema kwa wakati huu, hata ikiwa Katiba yetu itapitishwa, tutatumia Electoral Commission ambayo iko kwa wakati huu. Tumeangalia vyama vya kisiasa na pia utawala. Tumeangalia pia jinsi mahakama itakavyoweza kutoka katika hali ya wakati huu kuingia mpaka wakati ambapo tumetoa mapendekezo, na tumeangalia pia haki ambazo zilikosa kuzingatiwa na jambo ambalo litakalofanywa. Tumependekeza kwamba Tume ya haki iweze kufanya uchunguzi na kuweza kupendekeza mambo yatakayofanywa pale ambapo kulikuwa ama kulikuwa hakukutendewa uhaki. Tumeangalia pia mambo ya ardhi na pia jinsi ambavyo tutaweza kutekeleza mambo ambayo yamependekezwa kwa Katiba.

Asanteni kwa kunisikiza, kwa kifupi, hayo ndiyo mambo ambayo tumeyapendekeza katika Katiba yetu mpya, na tungewakaribisha kwa wakati huu kwa wale ambao wana maswali au mambo fulani ambayo wangetaka nifafanue au wana mafikira fulani kuhusu hii Katiba. Tafadhali wazungumze, na tunawaalika mfike hapa mbele mtupatie majina yenu. Mzungumuze mkitumia microphone ili watu wote wawasikize na tuweze kunasa sauti zenu kwa kuweze kuwandika report baadaye, na hatimaye nitajaribu kuwajibu hayo maswali. Ukimaliza utajiandikisha pale. Kuna Bwana Mukewa ambaye atataka jina lako.

**Gideon Mutiso:** Asante sana. Madam Commissioner, kwanza nitoe jina langu. Mimi majina yangu ni Mheshimiwa Gideon Mutiso, ambaye ni mwanzilishi kwa Constituency hii tangu nyakati za uhuru ndiyo nilikuwa Mbunge wa kwanza na pia nilikuwa katika harakati za uhuru, kupigania uhuru wa nchi hii. Wakati huo nikiwa Nairobi katika chama ambacho kilikuwepo kabla ya Kanu kilichokuwa kikiitwa Nairobi Peoples Convention Party ambacho kilikuwa kinaongozwa na marehemu Tom Mboya, na mimi nilikuwa mweka hazina wa chama hicho, na hicho ndicho kilizaa Kanu. Sababu ya kusema mambo hayo ni Kwasababu, nimesikia mambo mengi ambayo umezungumza, na nasikitika ya kwamba sitakuwa na muda mrefu Kwasababu kuna mazishi yanaendelea na niya jamaa ambao tunahusiano sana. Wamemaliza misa hapa katika kanisa na sasa wamekwenda nyumbani. Nitapitia tu kwa haraka sana mambo ambayo nataka kuzungumza, halafu mtaniruhusu niende huko, sitasikia majibu yako.

Kwanza nimefurahi sana kwa jinsi ulitoa maelezo ya Katiba mpya na kwa lugha ambayo ilikuwa ikieleweka kabisa, na kwa sauti nyororo ya mama ambayo nafikiri kila mmoja wetu amesikia bila tashwishi yeyote kwa maneno ambayo ulikuwa ukiongea.

Nimefurahi sana mimi na vile umeeleza vile mmefanya. Kitu cha kwanza ambacho ningependa kusema ni kwamba kwa ufupi tu, nimeona katika Katiba na umeeleza, nimeonelea ni lazima Chief Justice au Mkuu wa mahakama awe ni yule ambaye ni Senior Judge na qualifications zile zingine ambazo zinastahili. Sio kama vile ambavyo tuko sasa, na kwa hivyo hio ni jambo

ambalo nawapa hongera sana, kwa kufikiria jambo hilo maanake nakumbuka ya kwamba wakati Chief Justice wa sasa alipo teuliwa kulikuepo na mzozo, na kwa hivyo Kwasababu yeye alikuwa Public Prosecutor na kulikuwa ma-Judges on the bench na hawakufikiriwa, na kukawa na mzozo lakini ukaja ukatulia. Kwa hivyo, natoa hongera sana kwa vile mmeonelea jambo hili ni lazima lifuate utaratibu wa experience na kujua kazi katika pahali ambapo unafanya kazi.

Jambo lingine ni vile mmesema ni lazima kuweko na siku tatu muhimu katika nchi ambazo ni national days. Mlisema June first ama tarehe mosi June, siku yote ya Madaraka ni siku muhimu sana, mkatoa pia siku ya Jamhuri tarehe kumi na mbili December, halafu ya tatu mkasema ni siku ya Katiba, ambayo pengine ilikuwa imewekwa ikifananishwa kama Kenyatta Day na mkaonelea ni vizuri watu wataamua itaitwa Katiba Day ama itakuwa vipi, ama itaendelea kuwa Kenyatta Day. Kitu ningesema pale ni kwamba maoni yenu ni ya muhimu sana, maanake Kenyatta Day haswa haionyeshi kwamba kuna watu wengine ambao walipigania uhuru, isipokuwa marehemu Kenyatta mwenyewe. Ningependa kukujulisha kwamba sisi ambao tuliweka hiyo tarehe, tuliweka kwasababu kulikuwa kuna upinzani mkubwa sana wa wakoloni, wakati tulikuwa tukiendesha harakati za ukombozi katika chama hiki nilisema, Nairobi Peoples Convention Party. Tulikuwa tunataka kuweka siku ya Kenyatta iwe muhimu Kwasababu wakoloni wakikuwa wakisema wanataka kupeana uhuru without Kenyatta.

Kwa hivyo, tukasema lazima hiyo siku itambulike na tukaichukuwa kama ndiyo siku ya revolution day, ambayo Kenyatta alishikwa na wengine na kuimaanisha sana ndivyo hata wakoloni watambue ya kwamba tunampenda Kenyatta, ili uhuru upatikane na hatuwezi kupata uhuru without him. Hii ndiyo ilikuwa condition ya kwamba hatuwezi kupata uhuru without Kenyatta. Nakumbuka ya kwamba wakati Lancaster House wajumbe wa Legco walikwenda, ili mbidi Kariuki Njiri, the late, amuondokee Kenyatta kiti hapa Muranga, ili aweze kuongoza ujumbe wa wajumbe kwenda Lancaster House. Kwa hivyo, hiyo siku tukiibadilisha, kwangu sioni ubaya wowote, iambatane na uzito wa mafikira za leo.

Jambo jengine mmesema ya kwamba mwananchi wa Kenya anaweza kuwa mwananchi wa nchi nyingine, na hiyo kwangu vile vile naunga mkono Kwasababu kulingana na vile ulimwengu wa sasa ulivyo, si kama vile ilikuwa nyakati zile kabla ya uhuru. Ni watu wengi wamekwenda Amerika wanapewa ile green card wanakuwa wananchi wa huko, na kwa hivyo huku pengine wanapoteza haki zao. Kwa hivyo mtu akiwa anaweza kuwa mwananchi wa nchi hii na ingine, kwangu sioni ubaya Kwasababu huu ndio mtindo ambao unaendelea katika ulimwengu.

Jambo jengine ambalo umesema ni juu ya haki za mtu. Mimi Madam Commissioner, unaponiona hapa, ni moja ambao nilidhumiwa sana na sheria za nchi yetu. Nilifungwa mwaka wa sabini na moja, miaka tisa na miezi sita, na sikufungwa kwa jambo jengine, isipokuwa kwa kutetea watu ambao walikuwa wamenichagua kama mjumbe na kusimama katika haki, lakini nikanyimwa haki ya kuwa hata na wakili na nikasukumwa tu gerezani bila kufikiria haki za mtu. Kwa hivyo hiyo ikiwa sasa inaelezwa katika Katiba ya sasa kwamba mtu lazima haki yake ifikiriwe, ikiwa mtu ameshikwa apewe nafasi ya kuwa na wakili wake na ichunguzwe bila kudhulumiwa, ionekane ana haki ama hana haki, hiyo ni jambo muhimu sana.



Jambo jengine ambalo mmesema ni juu ya kuabudu Mungu. Mmesema ya kwamba mmetoa uhuru wa kuabudu. Pale nina swali ambalo pengine ningependa ufafanue baadaye, kwamba hamkuenda mbele kabisa ku-define ni Mungu gani, maanake tunajua kuna watu wanaabudu shetani Kenya hii nimesikia maneno hayo, na Kwasababu mmesema kuna uhuru wa kuabudu, huenda ikawa mtu akiwa ni dini yake hiyo na anaabudu shetani, huwezi kumpinga kisheria, maanake anasema yule ni Mungu wangu. Kwa hivyo, iwe defined kwamba ni Mungu yule wa haki, one true and living God, si mungu wa kibinadamu ama shetani.

Ile ingine ambayo ningependea vile vile kuuliza, nilisikiliza na sikupata, kuna uhuru wa madini kuendelea, na tunavyo ona sasa kuna mtindo mwingi sana wa madini. Mtu akikosana na viongozi wake katika dhehebu yake ambayo yuko, anatoka anaanzisha ingine. Pale akikaa na mwingine anatoka. Zimejaa dini za aina hiyo. Kitu ambacho nilikuwa nataka kuuliza, ni kama mngefikiria kama kuna limitations to how many religions tunaweza kuwa nazo ama ni nini, not real religions, lakini madhebu, ni mangapi ambayo yanaweza kukombolea kwa Katiba iendele na kuwandikishwa, maanake mwandikishi wa madhemu haya hana protection. Mtu akija aseme kuna haki ya kuandikisha dini na yeye hana dini yake anatoa jina lolote tu, yule hawezi kumpinga. Kwa hivyo, maoni yangu ni kwamba kuwepo na limitation maanake ukiangalia sasa, madini ambayo yako Kenya hii ni mengi sana, na mengine sina hakika nayo sana. Siwezi kusema, lakini ni vile tunavyona. Kwa hivyo, hilo ni swali moja ambalo ningekuwachia, muone kama kuna kitu ambacho kinaweza kufanyika juu yake.

Ile ya mwisho ambayo mmesema ni juu ya political parties kupeleka returns. Hiyo ilikuwepo hata kabla ya uhuru maanake nimekueleza kwamba tulikuwa na vyama, tulikuwa na chama kati wakoloni walikubali tuanzishe political parties on district basis, 1958 baada ya Ghana kupata uhuru '57. Tulikuwa na easy returns, hata za vyama wafanyakazi, ni lazima kila mwaka utoe returns, uonyeshe nimepata pesa ngapi, watu ni wangapi na return ama officials ni wakina nani, lakini hii sasa imepotea. Mkiwa mnairudisha hiyo, pia hata mimi naiunga mkono maanake ndiyo inaonyesha kwamba, chama kitakuwa kikifanya kazi. Kwa hivyo, kwa hayo, ningesema mambo mengi lakini, muda ndio .....(end of tape).

Kama mtu alikuwepo wakati uhuru ulikuwa ukipiganiwa na kama mmoja wa wapiganiaji wa uhuru na ni kama Mbunge wa sehemu hii nyakati hizo, na mpaka 1957 ndiye nilikuwa nimetoka kidogo isipokuwa sasa wananchi wamenisukumma sana wakaniambia ni lazima nirudi katika uongozi, nakuambia, hii ni jambo muhimu sana la kufikiria, kuona ya kwamba Katiba hii ambayo mmetoa hii mpya, mimi kwangu naiunga mkono, na nafikiri kila mtu ambaye ni mtu ako na right thinking mind, ataona ya kwamba Katiba hii ni lazima tuikubali hii mpya, maanake tumetoa pesa nyingi kuitengeza na haina maana kuja nyakati za mwisho kuwaza kusema ni mbaya, kwa hivyo mimi na-unga mkono kwa kila kitu ambacho mmefanya. Asante sana.

**Samson Ndolo:** Ninasema ni asante sana kwa mwenyekiti wa Katiba, Madam. Ile mambo umesema juu ya Katiba... jina ni Samson Muia Ndolo, kile kitu ambacho nimesikia ambacho mmesoma nikakosa kusikia vizuri, maneno yote ni mazuri ambayo yale umetusomea juu ya Katiba mpya, ijapokuwa ni upande mmoja. Upande wa hawa watu ambao wanaitwa advocates sijasikia kama kuna masharti juu yao. Sababu ya hiyo, hawa ma-advocates unawapa kazi akutetee asimamie kesi yako juu ya

makosa fulani, lakini kesi akipatiwa, inaweza kuchukuwa muda wa miaka mingi sana. Pengine kwa mfano, anaweza kukuambia kesi yako, watu ambao wale wa-insurance ambao wanaweza kulipa mtu akiwa ameumia, wamesha amua uweke sign juu ya pesa fulani ulipwe. Hiyo karatasi ambayo utaweka juu sign ndipo ulipwe, utaweka sign na sign yake itakuwa iko na ya mwenyekiti wa insurance ambao watu wale wanalipa iko, hiyo inakiwa ni ma-sign tatu. Saa hii wewe unaweka sign unakwenda kungojea nyumbani uletewe barua juu ya cheque ya pesa yako na unaweza kungojea miaka na miaka. Baada ya kungojea siku nyingi, ukose kupata hiyo ya ma-sign yako ni nini, halafu inaonekana anakusukumma uweke sign aende akapewe cheque ndivyo akatoe pesa aweke banki yake. Ie kitu ya kushangaza, hiyo pesa atakwenda kupewa, ni yeye aliumia au ni mimi niliumia? Hiyo ni swali ambalo mimi sijasikia kama juu ya ma-advocate, kama kuna masharti fulani yamewekwa, ijapokuwa kuna mahali hiyo ma-case inapelekwa na mtu akiwa amekosana na advocate wake, kumlipa pesa yake. Kuna mahali ambapo hiyo ma-kesi inapelekwa, lakini anachukuwa muda mrefu sana. Mimi sijasikia kama kuna masharti amepewa akifanya hivyo, kama anaweza kunyanganyua barua yake ya advocate, ama namnagani isijapokuwa uliseme advocate ndiyo advocate lakini sijasikia masharti yake. Nime-koma hapo.

**Col. Mativo Elijah:** Thank you very much Madam Commissioner, my name is Col. Mativo, Col. Elijah Mativo. I have a few observations on the document. First of all let me commend the Commission for giving us such a good new Constitution. When I look at the chapter on Public Service Commission, that is Chapter 14, it is not a serious observation, but it is just a remark or rather the wording. Madam Commissioner, we know very well that there is a problem of employment, and hoping that this Constitution will improve the economy, I feel that we should also improve the terms of employment How do we do it? Under part one, that is Chapter 14 part 1 (i), it is worded “reflection of ethnic composition of the population in the composition of the Public Service at all levels”. Mimi ningeonelea hapo, recruitment into Public Service should be on district quota basis, and the Constitution should reflect it without any complications. Kwasababu hii ni a sitting statement, what is there is a reception statement, and we know once the Constitution is in place, it will be very difficult to change it. So, let recruitment of public servants, the recruitment of students to public colleges, be based on district quota, that is what I mean.

Madam Commissioner, the Constitution should also reflect on the recruitment of the members of the Armed Forces and the Police. Again, this should also be based on district quota, because we know those two services, that is the Defence Forces and the Police are very important ingredients of our nationhood. In the Constitution, I do not know whether it is an oversight, but there is no mention of the National Security Intelligence. I do not know whether it is an oversight, or it was left deliberately but I thought that, that organization should also be reflected in the Constitution, the National Security Intelligence.

I am a retired member of the Armed Forces, and I have another serious observation to make. The appointment of the Chief of General Staff and the three service Commanders, that is the Army Commander, the Air Force Commander and the Navy Commander, Madam Commissioner, we have witnessed previously, appointments being made on tribal basis. Let us avoid this in future because we do not know the Presidents that we are going to have in future, how they will be. Cover it in the Constitution, that the appointment of these service Commanders be by the President, okay, but approval be made by

Parliament, so that we have some genuine appointments. Elsewhere like in the United States, the service commanders are appointed, and the Congress approves. It is also important that we adapt that one.

I also have another point on the National Days. I feel that we should also adapt an Armed Forces Day just like it is elsewhere. This can also be combined with the Hero's Day, and it should be the day when the nation sees their military might, because we know to defend the Constitution there must be an Armed Forces, to defend the country properly, to defend our economy within the Armed Forces. It is the pride of the Nation, so it is important that we have an Armed Forces Day as a National Day.

Under the Chapter you have mentioned the older members of the society, you have not given any definition of who is an older member of the society. I feel we should say, let us say a fellow who becomes 50 years old qualifies to be an older member of the society. This is because it does not give any age limit. If we put it that way, it will be clear. It will be clear as to who is an older member of the society. Elsewhere again like in the United States, once you reach the age of 50 years you qualify to be an older member of the society as a senior citizen; you have that respect. Thank you very much.

**Julius Kilela:** Madam, nataka niseme asante sana kwa nafasi hii. Kwanza ningeshukuru kazi yenu. Kwa majina naitwa Julius Kilonzo Kilela. Nimekuja hapa kuuliza swali tu, na kabla ya swali langu, ningetaka kujieleza kidogo. Mimi ningependa kusema nilikuwa mmoja katika wakati wa kupigania uhuru miaka ya 1955 nikiwa kijana wa umri wa miaka kumi na tano huko pande za Embu. Nilikuwa kijana wa kupelekea Mau Mau chakula mistuni, pamoja na baba yangu. Kwa wakati huu, mimi ni mwalimu mstaafa. Niko huko kwa kijiji nikiendeleza mambo ya village development na wenye vijiji, na mambo ya clans, mambo ya ukoo. Nimesema nimekuja hapa kuuliza swali. Swali langu ni juu ya customary laws. Sijasikia vile nyinyi kama Commissioners mmependekeza kuhusu customary laws na unajua hizi ziko nyingi kwa kila kabila, na sasa sisi Wakamba, tuko na customary laws kwa wingi na nyingi zake ni za muhimu. Ningependa kuuliza, nyinyi kama Commissioners, mmefanya nini kupendekeza upande huo? Asante sana.

**Benjamin Kimei:** Asante Madam Commissioner. Kwa jina naitwa Benjamin Kimei Mwatu, na mimi ni mwalimu. Ningetaka kugusia Chapter 2, item number 13, ile inagusia juu ya National Days. Hapo kuna hili swali la Kenyatta Day, iwe Kenyatta Day ama iwe Hero's Day. Mimi ningependelea kama Mheshimiwa Mutiso amesema, hii Kenyatta Day igeuzwe iwe Hero's Day, namuunga mkono kabisa iwe ikiitwa Hero's Day kwasbabu ni wengi, akina Ngei na wengine ambao walifungwa na hata wengine majina hatukuwambiwa, lakini tunaambiwa kulikuwa na ..... Wakawekwa katika kizuizi. Kwa hivyo, sio Kenyatta peke yake, hata sio akina Ngei peke yao, kulikuwa na wengi, na wale ambao walionelea igeuzwe iwe Hero's Day, na waunga mkono.

Kuna hili swali la Katiba Day hapo hapo, Kenyatta Day iwe Hero's Day ama iwe Katiba Day. Vile vile hiki ni kitu kizuri. Kama tunaonelea tuwe na ...siku ya Katiba Day, sijui iwekwe siku gani. Kuna mwenzangu hapa amesema ya kwamba anaonelea tuwe na siku ya Majeshi, lakini tuna huduma nyingi sana za muhimu katika Kenya, na tukiangalia katika kila huduma,

tunaona umuhimu wake. Kama mimi ni mwalimu, ningesema hata kuwe na siku ya elimu, Kwasababu hata yule mtu wa Jeshi, ya kwanza anaitishwa barua ya mwalimu. Kama unatakiwa kazi fulani, utaitishwa degree, utaitishwa diploma, na wewe hiyo umepitia kwa mwalimu, kwa hivyo walimu ni muhimu sana kuliko hata mambo mengine yote.

Katika Chapter ya tano, Chapter 5, Item number 32, Clause 2, inahusu jambo ya right to life. Hiyo ndiyo katika Katiba watu walipendekeza na mkapendekeza ya kwamba hii hukumu ya kifo iondolewe. Lakini hapo nina swali. Kuna nchi zingine kama America na Europe, na waliondoa hiyo hukumu vile vile, hata nikisoma magazeti naona, lakini wanaendelea na kuwa watu hata ingawa wanawekwa katika kiti kile wanaita electric chair, na unauwawa. Kwa nini hata wameenda mbele na wakarudisha hiyo? Kuna ile deliberate killing, kwa mfano juzi tuliona kuna Mu-amerika aliuwa wanawake wengi, na hakukuwa na sababu yoyote, lakini aliona ni vizuri hiyo. Hii maisha ya hawa watu aliuwa na hii yake, kwani yake ni ya muhimu sana kuliko ya hawa? Kwa hivyo kama yeye anaua hata yeye. Ninasema, hii iangaliwe sana. Sheria hii itolewe kabisa. Naonelea iweko, lakini ichuguzwe sana kabla haijatekelezwa Kwasababu kama hiyo inaweza kutumiwa vibaya na watu wengine, directly or indirectly.

Katika Chapter 8, Item number 156 (B), inaongea juu ya umri wa Rais, na inasema Rais asizidi miaka sabini. Madam Commissioner, mimi sikubaliani na hiyo, na ninakata Kwasababu pengine hii inapendekezwa na watu walikuwa wanaogopa ile uchaguzi inaendelea, kwa hivyo mtu akaona nikiweka hii ni mtu fulani atazuiwa. Nasema hivyo Kwasababu, tukiangalia katika nchi fulani nyingi za ulimwengu, kuna mawaziri, kuna ma-President ama waziri ama viongozi wa nchi wana miaka hata 76, 80, na wanaendelea vizuri kuliko hata vijana wa miaka arubaini ambao wamhangaisha nchi zao. Kwa hivyo Kwasababu tunasema uongozi ni ki-power, sionelei muhimu ya hiyo part hapo, ilo tu kama wananchi wana macho na wanaonelea na kama wanaona mtu hata akiwa na 75 ama 76 ama 78 na anastahili kuwa anafaa kuongoza, humu sioni kuwekwa hiyo haitusaidii. Ile iliwekwa huko, pengine wale walikuwa na dhamira fulani. I do not think they had a good will. I do not know what to say, lakini sielewi kama itasaidia. Kwa mfano, tuna Carter, niliona juzi alipatiwa Nobel Prize, na ni mtu mzee sana na ni kati ya yale mambo mazuri anafanya katika ulimwengu kuleta amani. Kuna wengine hata vile vile nimeona wengine wakiwa na 80 na wamepatiwa hii Nobel Prize kwa kufanya kazi mzuri sana, na hawa watu hata wamezidi hiyo umri wa miaka sabini, wale wa juzi walipatiwa Nobel Prizes. Kwa hivyo hiyo, sionelei kama itatusaidia, pengine kuna watu vijana vijana pengine wamepenya katika Commission, na kutaka kuzuia wengine Kwasababu wanaona ni vitisho kwao.

Katika Chapter 10, Item number 216, kuna hii Village Government na yako haielezi ni nani atakuwa Chairman, atakuwa Administrator ama Chairman sijui kama nimuite Administrator namna mnamuita katika Katiba hii makaratsi hii ya draft Constitution. Kwa hivyo, nafikiri hiyo Draft Constitution iseme is somehow silent on who should be the Chairman, or how should he be, because in any organization, ni lazima kuwe na kiongozi. Sasa kiongozi wa hii haelezwi atakuwa nani, ama atachaguliwa kwa njia gani. Hapa katika hiyo Katiba Draft Constitution nimeona mnaongea juu ya Local Authority, Local Government na nikiangalia sana, ni kama hii Local Government, Local Councils ni kama zimeondolewa ni kama tuna hiyo tunaita District Government. Kama kuna Local Authorities, Local Government kama imeelezwa huko, I think that the Constitution is somehow silent on them. So, I would need just a bit of clarification there, that is the Local Authority, will they be

there or they will not be there.

Kuna Chapter 12, Item number 240(B), na hiyo inaingia juu ya environment management. Hapo sasa kumekuwa na shida nyingi sana. Unaenda unakuta wakati wa demarcation kuna watu sehemu zao zilikuwa na maji, na katika sehemu kama hiyo ya Yatta ile ni ile Nyari unakuta hayo maji sometime kunakuwa na wakati katikati ya mwaka inakuwa maji ni taabu sana kupata, na huyo mtu anaweza kutuuzia yale maji, na hiyo sehemu haikutengwa kwa watu. Kwa hivyo, nilikuwa nikitafuta kama kuna usaidizi wa Katiba sana juu ya hii scarce resources, is the Constitution saying anything about these scarce resources which should be used by all of us, because to buy water by some people is a problem. Hata kuna zingine, hii changarawe, unakuta sehemu ya mto inaenda mpaka kuinama huko katika ile mianda, na there is that sand just within the river beds, na hiyo sehemu, unakuta wakati wa demarcation haipatiwi mtu yeyote, ni sehemu ambayo inaachwa. Lakini, ukienda kuchukua hiyo changarawe huko, mtu anakwambia ununue na haiko katika sehemu yake katika map. Ndiyo sehemu yake inaendea huko, lakini katika map ukiangalia katika ile demarcation map ya land, haiko katika sehemu yake. Sasa, inakuwa shida kwa wale ambao hawana pesa nyingi, na sehemu zao haziendi mpaka kufika huko. Kwa hivyo sijui utatuambia nini juu ya hizi resources, natural resources which we normally use all of us.

Katiba nimeonelea kuna maswala ambayo imekuwa na shida sana. Lile swala ambalo hapo hata hapo awali imekuwa ni shida moja ni juu ile PTA na BOG katika shule. Hiyo I will not quote any Chapter, because it is not appearing there. Kuna hii PTA na BOG, na watu wengi walikuwa wameongea juu ya PTA na BOG, Kwasababu BOG wanajufanya ndio managers katika secondary schools, na PTA wanachaguliwa lakini they do not manage the school, na hapo awali tulikuwa tumeambiwa katika Katiba mpya, pengine huenda PTA wale wamechaguliwa na PTA ndio watakuwa managers wa mashule. Sasa hiyo iko katika Katiba ama iliachwa, na ningeonelea kama haiko, iongezwe katika Katiba. PTA members wawe ndio viongozi wa mashule, Kwasababu ndio watoto, na ndio wanatoa pesa wenyewe, na kama wanatoa pesa na kufanya jambo lolote, wana jukumu ama hukumu yakuuliza hii imetokea amaimefanya nini, ama inaendelea namna gani. Na vile vile juzi tuseme tangu mmeongeza hii TSC, nimeona katika hiyo Commission wameongeza TSC, na juzi wametoa kijitabu ambacho kimeeleza. Vile vile kumekuwa na Primary School Board, na kuna ile School Management Committee vile vile, na hiyo tulikuwa tanafikiri itakuwa katika Katiba hii mpya, itueleze kazi ya Primary School Board itakuwa nini, na kazi ya School Management Committee itakuwa nini. Kwa hivyo, hivyo vitu vyote, management ya mashule yetu haikuongezwa katika Katiba. Je, tutaipata mahali pengine ama namna gani? Asanteni.

**Issac Peter:** Nitachukua fursa hii na kushukuru Madam Commissioner kwa kupata wakati hasa kututembelea hapa Matuu, nashukuru sana. Mimi naitwa Issac Mbipita kutoka hapa Matuu. Mawazo yangu si tofauti sana na vile watu wengine waliwahi kugusia mambo muhimu yanayohusu Katiba, isipokuwa nitataja tu mambo mawili, matatu. Kwanza kabisa ningependa kugusia hii swala la National Holidays. Kusema kweli kama hatutaandikisha Kenyatta Day kuwa kama siku ya kihistoria katika historia ya Kenya, kwa njia moja haina nyingine, huenda tukapuuza ushujaa wa huyu Mzee, na taifa nzima kwa jumla. Maanake hata katika kipifu cha ufanyiaji wa mitihani, mwanafunzi huwa anadaimiwa, ni nani aliyekuwa mwanzilishi wa taifa hili na moja kwa

moja mwanafunzi bila kuharibu wakati, husema nia yake Mzee Jomo Kenyatta. Kwa hivyo kwa njia moja haina nyingine, huenda tukaanza kutatanisha historia ya siku hii. Jambo tu la kugusia, nitasema, kama itawezekana, kumbuka tulikuwa na Katiba ya kwanza, na hii si Katiba mpya, ni marekebisho tu yameingia katika wamu hii ya pili. Kwa hivyo, kama tutapatia Katiba ya pili nafasi, pia tukumbuke zaidi historia ya siku hiyo.

Nitaenda katika pendekezo la pili ambalo linagusia umilikaji ya ardhi na mali. That is fundamental rights and freedom kwa zote zote mbili, wanaume na wanawake. Utakuta kwamba Katiba imegusia usawa baina ya wanaume na wanawake, na mimi kwa tashira na kumbu kumbu nitarudi tu kidogo, nigusie Bibilia ile inasema. Katika Bibilia, mwanaume aliumbwa kwanza. Hali kadhalika, mwanamke alifuatia, na Bibilia inataja vizuri sana kuwa mwanamke aliumbwa kama msaidizi. Hivyo basi, mwanamume alikuwa ajisaidie, na akapewa tu msaidizi. Kwa hivyo, tukiwapa fursa ya kwenda na mbele ama usawa katika jamii, huenda tukaleta madhara kama vile, tutatatanisha mi ko ya kitamaduni, that is customary law, kwa vile kama kwa mfano, mwanamke kama ameolewa, huwa kwa kawaida tunajua yuko katika mamlaka ya mzee wake, na si katika nyumba hata kijiji, na pengine taifa nzima kwa jumla.

Sisemi wanawake wasipewe nafasi kuchangia katika kila nyanja za maendeleo yeyote, lakini lazima tuchunguze na tuangalie kama kweli kutakuwa ni usawa ama tutatumia lugha nyingine. Maanake tukisema ni usawa, kwa kimombo tunasema equality, actually is the same on both sides. Kwa hivyo kama tutatumia lugha ingine, itakuwa tunaelewa kidogo maanake mwanamke kawaida huwa chini ya mwanamume. Samahani mimi sijaoa, na karibuni nitaenda nitaoa. Kwa hivyo lazima hili jambo tuangalie, kwa vile mwanamke anafaa kuwa na unyeyekevu. Kama tutapewa hatua sawa, hapa italeta shida kidogo. Tukiangalia mambo ya kiutamaduni kama vile miiko ya Wakamba, customary law ya Wakamba, mimi ni Mkamba halisi, utakuta kwamba zamani wanawake hawakupewa nafasi ya kuchelewa nje kabisa wakati mwingi sana, na hawakuweza kupata nafasi ya kuchangia katika mambo ya kisiasa, mambo ya kimaendeleo zaidi, lakini walipewa tu nafasi ya kuchangia tu kulingana na vile Mungu aliwaomba. Hivyo basi Madam Commissioner, lazima hii jambo lifikiriwe kwa undani kidogo. Siwadumishi, kumbuka ni viumbe, lakini tunapotumia hilo jina la usawa baina ya pande zote mbili, jameni tuangalie hapo.

Tukigusia katika mambo ya utawala, Locational Government, pia Tume ya Katiba imeinua wanawake kwa njia moja haida nyingine, kwa vile tumeona wanawake wamependekezwa kuwa wawili katika Location kuwakilisha pengine shida ama disputes za hiyo Location, na hatukupewa ni kwanini Tume ilipendekeza wawili wala Tume ilinyamaza, haikugusia ni lazima wawe na miaka mingapi, hata kama ni wanawake wawili. Je, walipoketi chini na kuona nafasi zitolewe mbili za wanawake, hawakufikiria wanaume sasa wako? Tuseme kwa mfano, mwanamke ameenda kutatua disputes huko kando na ameolewa na pengine ni nyanya tu anelewa na haya mambo ya mipaka na shida zingine ambazo zinahusu jamii, sasa akichelewa huko nje katika nyarakati za kwenda kutafuta solution, utakuta atakuja nyumbani akute mzee wake pengine ame-boeka, mzee hajakula asubuhi, wajukuu wanarandaranda huku na kule, kwa hivyo lazima tuangalie haya mambo, yaende pamoja na vile ulimwengu unaenda. Nashukuru, asante.



**Com. Ali: (inaudible)**

**Titus Mwaniki:** Nashukuru Madam Commissioner, kwa kututembelea ili kutupatia reporti ya vile tulipendekeza all over the country, na tunasikia actually in some of...

**Com. Ali: (interjection)** What is your name?

**Titus Mwaniki:** Titus Mwaniki. I am a businessman, ninafanya biashara hapa Matuu. Yangu tu ya kwanza kuongea nikushukuru vile umetutembelea na vile mliweka kulingana na maoni ya wananchi. Sana sana ninashukuru upande wa Administration, upande wa Provincial Administration. Actually the way it was put mimi nasema hivyo ndivyo vile tulipendekeza.

Nilikuwa hapa wakati wa mapendekezo na nilipendekeza kitu kama hicho, na ninashukuru Kwasababu my point was included, so hapo ninashukuru sana.

Ile ingine sasa, mambo ya Katiba inaendelea kummalizika ama inaendelea kupatiana kwa wananchi ili mambo yale mengine yaweze kuendelea. Tuko na shida pia katika wakati huu ama wakati ujao. What will happen kama Raisi yule ako kwenye kiti, mapendekezo mengine yale mmeweka kule ndani kama ya Prime Ministers and the other powers ambayo presently hayako ndani ama hayako katika serikali, akiona mambo mengine ni mazito ama yataweka uzito kwa serikali na aweze kusema haya mambo yameingia lakini sionelei kama wale nitakao wachia serikali kama wataweza uzito huu kuupanga na aweze ku-reject some of haya mapendekezo asema meingine ni kama hatakubali na aweze kutoa yake ama aweze kukosa kupatiana. Kunao uwezo wenu wa kuweza kushauriana na yeye ama mtakubalia tu vile yeye ataweza ku-instruct?

Ile ingine, ningeweza kugusia ni wakati wa uchaguzi, kunakuwa na shida. Kuna shida ambayo inakuwa. Kunao vijana ambao wanatengwa na maybe na vyama tofauti, ama vijana wanatengenezwa ili kuvuruga amani wakati kunayo mikutano ya siasa. Katika Katiba vikundi kama hizo mumepatia wale wanaoshikilia upande wa usalama jukumu ya aina gani ili hao vijana ama wale wengine wanaohusika kwa kuvuruga ama ni wakati wa uchaguzi, Kwasababu it is there. Hatuwezi kusema ati hawa vijana ni wa kikundu fulani, hawa wengine ni wa kikundi fulani, ni wa ukoo fulani ama ni wa kutoka katika kabila fulani, hii wako. Nashukuru.

**Com. Ali:** Kulikuwa na mtu mwingine?

**Francis Kivuva:** Kwanza ningeshukuru sana ma-Commissioner. Kwa majina naitwa Francis Chalo Kivuva. Ningetaka kugusia jambo moja. Naona kunashida sana wakati wa uchaguzi hasa wakati kura zinaendelea. Sijui kama kuna hatua ingechukuliwa kuwagalia kwamba kuna vikundi ambazo zingetengwa kuangalia kila chama cha uchaguzi, maanake wakati tunachukua serikali iangalie mambo ya uchaguzi, naona hapo kunakuwa na shida kidogo sababu hii serikali, chama kina chotawala ndicho sana kinagusia serikali. Kwa hivyo, naona serikali hapo inagusia sana chama ambacho kinatawala. Kwa

hivyo naona hiki chama kinatawala kita dumu kwa maisha, Kwasababu sasa kama serikali itakuja kila wakati ndiyo inasimamia hali ya kupiga kura, itakuwa tu inaangalia hawa wa hiki chama ambacho kinatawala kwa hivyo wapinzani wakuwa wanachoka bure. Hapo ningepomba tupunguziwe kidogo, waone kama kunawezekana kuwa na kundi ambalo, ama makundi ambayo kila chama itakuwa na tuseme serikali yake ambayo kitakuwa inaangalia tuseme kura, kuhesabiwa kwa kura, na mambo kama hiyo.

Ile ingine ningepuliza ni swali, sijui nyinyi kama Tume mtachukua hatua gani kuona tumepiga kura kwa Katiba ambayo sasa, ama Katiba ambayo sasa mumerekebisha, tusikie kura kwa Katiba ambayo tulikuwa nayo hapo awali, na tunayo sasa. Asante.

**Elijah Mbaka:** Asante sana kwa Madam Commissioner, na ma-Commissioner wenzake kwa kuutembelea hapa Matuu. Kwa jina naitwa Elijah Mbaka, na labda I would want to address one issue ambayo umetaja kidogo, na sijasikia uzito wake. Maanake tukiangalia sana ndani naona, hiyo issue ndiyo inatusumbua sana hapa nchini Kenya na kama inawezekana, it is supposed to be addressed as national disaster number two, kufuatia ukimwi, na hiyo ni corruption ama ufisadi,. Nimesika ukitaja ya kwamba sisi wenyewe ndio na hiyo nyanja. Tunafaa kuwaangalia hii maneno ya ufisadi, kuangalia ya kwamba hujahonga, lakini kidogo pale ningetaka kusema ya kwamba ukiona mtu mwenye anaenda kuhonga, akiwa anahongana huwa mimi nataka kujinufaisha kibinafisi, ama nataka kuiokoa nafasi yangu ikiwa nimefinyiliwa mahali fulani.

Nimesikia ukitaja ya kwamba sisi wenyewe tunafaiwa labda nikikamatwa na niangalie hii kitu sio zito sana, nikubali nipelekwa mbele, labda nishtakiwe, maanake yule mwenye amenishika atanikamata, sio yeye atanihukumu. Lakini, tukiangalia vizuri ya kwamba hata wewe Commissioner, huwezi angalia kitu unaona kitakusumbua baadaye huifuatilia ndiyo uangalie mwisho wake, kwa manufaa ya wananchi wenzako. Kitu muhimu mimi naonelea ni kwamba hii Katiba mpya I-address hii issue deeply. Deeply ni kwamba kama itawezekana, I-introduce a special Anti Corruption Unit ambayo itafuatilia sana sana mwenye kuhonga, wacha mwenye kuhongwa. Maanake utaangalia haswa kwa magari, corruption imeendelea sana, tuseme sasa kwa matatu. Utaona ya kwamba sisi tukiwa ndani ya gari, hata hawa makanga ama madereva wa matatu hawatuogopi sisi abiria, hawajui sisi ni akina nani. Utaona tukifika karibu na roadblock ya Polisi, anatoa pesa, anakuja kuja kidogo na hajui ameketi na nani pale mbele. Anapea conductor ama mwenyewe anashika. Yeye kile anajua ni kwamba, kuhonga kwake kushikwa na kukamatwa si rahisi akihonga, lakini anaficha-ficha zile pesa ndiyo yule askari asionekane akifanya nini? Akihongwa. Mimi vile ningesema ni kwamba haswa haswa hii issue ya corruption, haswa naonelea hii Katiba hata zile details nyingi imeenda ndani yake ni kuhusu hii corruption, na ndiyo unaona sasa hata hii Provincial Administration ndiyo imekuwa ni very corrupt. To the extent kwamba imesemekana wacha tue na utawala aina mwingine. Ndiyo unaona kwamba kama ni mtu mwenye kuhonga, afuatiliwe na apewe adhabu kali kuliko hata zile pesa angetoa kuhonga. Ndiyo sababu utaonelea ya kwamba ukifanya makosa kidogo, utakubali upelekwe mbele maanake pale ukienda labda utatoa fine kidogo, kuliko kukamatwa ukihonga maanake hiyo ndiyo itakuwa adhabu kali sana. Asante.

**Margaret Kimeu:** Majina ni Margaret Kimeu. Asante kwa ma-Commissioner wenzetu na kwa washirika wote wale wamekuja hapa kuendesha haya mambo ya Katiba. Mimi ningetaka kusema, ningetaka kuunga mkono ile hali ya watu



wakurekebisha Katiba waliona wanawake wawe na usawa na wanaume. Hasa hasa hata sio kama mimi najitetea, mambo yangu pengine hata yameshaenda lakini, wale washichana tumewazaa, hata hapa sisi wote ni wazazi, kila mtu amezaa msichana. Hawa watoto wetu watakuwa na taabu kama hatuta-consider them. Kama tutasema wakae tu nyumbani kama zamani. Sasa unajua wanaume zamani walikuwa wanaoa wanawake watatu, na sasa wanaume wanaoa mwanamke mmoja wa ndoa. Wale wengine wanajitegemea. Sasa kama tutasema hatutaangalia mambo yao na hao wanataka kuendesha manyumba yao, sasa watafanya nini? Kama wote wataenda tusema hatutaki wakuwe na usawa na wanaume na wako na miji yao. Wengine wamesoma kama vijana, si wanaenda shule kijana anasoma, msichana anasoma, masomo ni ile ile tu. Mtihani ni ile hoja. Basi, tukisema hivyo hawa watafanya nini? Ninaomba mkono hiyo moja ya kusema wanawake wawe na usawa na wanaume ndiyo waendeshe manyumba yao yangu ni hayo.

**Jackson Muinga:** Asanteni Madam Commissioner. My names are Jackson Muinga. Swali langu linahusu utawala wa Locational administrators. Nimeonelea upande wa Districts kuna tena (inaudible) lakini upande wa Locational, ni kama sijaona kama kuna kitu kinaongea juu ya wakati wa-tahudumu kwa ofisi. Swali langu ni hili. Ikiwa kutakuwa na vile tumeona watu wa Council wakiwa elected na wanachaguliwa Kwasababu ni wazuri wanajua kuongea lakini kwa upande wa utumishi wanaangusha Councils na wanakaa miaka mpaka miaka mitano. Suppose, ikiwa kutachaguliwa mtu ambaye who is not development concious, hiyo Location itaumia kwa muda mrefu. Kwa hivyo, swali langu ni, kutakuwaje ikiwa tumepewa elected leaders in Locations, those are Locational Administrators, who are not delivering the goods, what will be done? Hilo ndilo swali langu. Thank you so much.

**Julius Muli:** Commissioner Madam, na washirika wenzangu, kwa jina naitwa Julius Muli, mimi ni mbiashara hapa Matuu. Pendekezo yangu nitarudisha kwa watoto, kulea watoto. Nilisikia kwa Katiba mpya ile pendekezo ya kulea watoto, tuele watoto wote, sawa! Hata wale wamepatikana nje ya ndoa. Sasa swali yangu ni hii, hawa watoto wanapatikana nje ya ndoa, sana sana wanafanya hata boma inabomolmoka, watu wanaachana. Itakuwaje kama huyu mtoto wa kutoka nje amekataa kusomeshwa, kuna pendekezo yaani serikali ingefanya kitu juu ya watoto kama hawa badala ya nyumba iporomoke? Kwa maana kwa pendekezo ya Katiba, nilisikia tu very lightly, wewe somesha watoto, lea watoto wote. Hii kitu hata nchi nyingine ya kupata mtoto yaani nje ya ndoa ni very serious. Hata unaona yaani wengine wakipata mtoto nje ya ndoa wanauwawa, lakini kwetu kwa Katiba yetu, inasemekana wewe lea watoto. Itakuwaje kwa hawa watoto wanapatikana nje ya ndoa ili tu-save boma hiyo isimalizike?

Ya pili, ninakuja kwa uridhi, mwanamke aridhi mali. Mwanamke nimekuwa naye miaka mingi. Tumekuwa na mali, na amekuja ametoroka na anataka ile mali tugawane. Aende pengine akatumie mali yaki huko nje na mimi ameniwacha hapa na watoto. Inawezekanaje yaani serikali iangalia kama yaani inaweza kuzuia huyu mwanamke asipate mali aende akaharibu, na sana sana wazee ndio wanawachiwa boma na huyu mtu anaenda huko pengine utamkuta Nairobi anakuwa yuko kwa club, yuko wapi, yuko kwa mambo yake huko na mzee hapa nyumbani anasumbuka na watoto.

Ya tatu ni pesa. Inaweza kupendekezwa namna gani, pesa isiwe na picha ya mtu yeyote, kwa maana utaona yaani wakati huu tunaelekea uchaguzi mkuu. Iko mtu tayari ameanza kufikiri nitaweka picha yangu kwa pesa namna gani. Kila .....baada ya miaka mitano tutakuwa tukienda tukibadilisha mapicha za watu, za watu, za watu. Inaweza kuchukuliwa kitu permanent, iwekwe kwa pesa tusije yaani tukaanza kupindua picha kila siku, kila siku baada ya election.

Ya mwisho, nitagusia ile watu wenzangu wamegusia hapa kidogo juu ya kifo. Hii sheria mumeonda yaani ya kifo. Kama mngetoa kifo, nafikiri kuuana itakuwa mingi, kwa maana nitaua mtu nikijua yaani sitauawa. Hata sana sana mtu akiuwa, tunatafuta advocate ili atetewe asiuwawe. Lakini sasa kama kifo hakuna, itakuwa yaani hata hakuna haja ya kutafuta advocate, wewe kwenda kule hutauwawa. Kwa hivyo yaani, fikiria sana. Mfikirie hii pendekezo ya kifo kwa maana kifo kitakuwa kingi sana. Asante.

**David Mativo:** Asante sana Madam Commissioner, kwa nafasi hii. Jina yangu naitwa David Mativo, na mimi ni mhubiri, ni deacon katika Kanisa. Ningependa kuuliza swali au ni fanye observation. Katika Constiution Chapter 5, Item number 44, 1 and 2, pahali inasema freedom of religion, belief and opinion. 44(1), every person has the right to freedom of concerns, religion, thoughts, beliefs and opinion. Two, every person has a right either individually or communally with others, in public or in private to manifest any religion or belief through or worship observance, practice or teaching. Nilikuwa hata wakati ule mwingine tulikuwa hapa, sikupata nafasi. Ningetaka kueleza ya kwamba siku hizi mambo ya worship yamekuwa mengine. Kuna watu ambao wameleta false worship or types of worship na wakiulizwa wanasema ya kwamba wao either wameota au wameambiwa na Mungu waabudu kwa njia hiyo. Kama vile tunajua kulikuwa na establishment ya core Commission ambaye ilikuwa ikaangalia mambo ya devil worship hapa Kenya, na tulijulishwa ya kwamba pengine ilipatikana, ilionekana kuna ukweli.

Kwa kweli kila mtu akipatiwa nafasi na hii Constitution Kwasababu tunajua itaenda mbali sana, si kitu cha siku moja au mwaka mmoja halafu iishe. Kuna wengine huenda ikawa wanakuja baada ya siku hizi waseme wamepata aina fulani ya kuabudu Mungu, na Kwasababu ni any kind of worship, wapatiwe nafasi. Hata ikiwa ni kula watu pengine kwa njia yaani aseme Mungu amemwambia awe anachinja watu, na kama vile tunasikia kuna wale ambao wanafanya ile human sacrifice wanapatia wengine katika nchi nyingine, wanaweza kupeleka wengine kuwafanya ni sacrifice. Kama Katiba ikiwa haina restrictions to a certain extent, pengine wale ambao wanaendelea na mambo kama haya nchi nyingine watatushika hapa kwetu Kenya, halafu waanze kufanya kile wanafanya au ile environment ya watoto, kama vile nimesoma kwa article moja katika gazette ati mtoto moja alikuwa defiled na mwanaume wa miaka ishirini na tatu pale South Africa akizingizia ya kwamba yeye anaabudu. Mwingine wa week tisa, week tano ati mtoto anafanyiwa mapenzi na mtu mzima na akiulizwa anasema anaabudu, ni njia yake ya kuwaabudu. Mambo kama hayo yanaweza kutokea hapa kwetu kama kila mtu akipatiwa kufanya kile anataka katika kuabudu. Hata tumeona wengine wameonekana, wengine wakifanya collections na ukimuliza anapeleka wapi hii pesa, anasema ni ya kufanya kazi ya Mungu. Ukisikia yale anahubiri, si maneno ya Bibilia, anaweza kuwa na maneno yake mwenyewe. Kwa hivyo, pendekezo langu ni ya kwamba kama hii Comission inaweza kufanya some restrictions iweke kiwango, siku sema kila mtu akiwa na any kind of worship anaweza kukubaliwa tu pengine wengine wanakuja na zingine ambazo nizakuumiza au zinaweza

kuwa si za kuabudu Mungu kwa njia ile ya kweli. Asante.

**Patrick Nzioka:** Asante sana Madam Commissioner, yangu ni swali. Majina ni Patrick Kyalo Nzioka. Kwanza ninawashukuru kwani mmefanya kazi mzuri. Vile nimesoma hiyo Constitution, ni vile tulisema hapa, some of us, wale walikuwa hapa. Kama vile nilisema, nimeona iko kwa Constitution so I can not say it is something which was brought. I said something and I have seen it in the Constitution. Yangu ni swali ndiyo nimesema. The Constitution talked about equality. I have no problem with the equality ama sina shida na equality lakini nimesikia mwanamke ametetewa upande wa watoto, that mtoto wa ndani ya ndoa ama ya nje wa ndoa asomeshwe. Sijasikia manamume akitetewa hapa. Supposing, how about a child, yule mtoto atazaliwa kwa maksudi that is, kwa maksudi mwanamke Kwasababu ametetewa ameambiwa mtoto atasomeshwa, ataenda kuibia mwanamume mtoto Kwasababu anajua atasomeshwa. Ataenda kuiba deliberately na sijasikia mwanamume akitetewa. What kind of a child he will educate. How about the children hii mwanamke atapata out of ndoa deliberately, ndiyo wasomeshwe na huyo mwanamume. Asante.

**Ambrose Kithumba:** Thank you very much Madam Commissioner, na maofficer wale wengine. Jina naitwa Ambrose Kithuma kutoka hapa Matuu. Hapa jambo ambalo ningependa kuzungumza juu yake ni moja. ...hii microphone inanisumbua(interjection) About the equality, or rather si equality ni uridhi wa mali na ardhi. Sasa Katiba ya Kenya inazungumza kimakini kabisa, na inasemekana kwamba our society should be a society that is free of many social evils kama tusema family disputes na vitu kama hizo. Hapa hapa mimi sina shida na msichana ama mwanamke akiridhi mali kwao. Lakini, ningependelea sana kama Katiba ya Kenya ingezungumza explicitly ama categorically, iseme ni mwanamke yupi ambaye ana haki ya uridhi wa mali. Kwani twaweza tukaona kwa mara mingi, wasichana wanaolewa wanakuwa wamama katika mafamilia ambazo ziko juu zaidi ya mandugu zake au ma-brothers wake. Wanasaidia nyumba ya baba yake zidi ya yule kijana na katika ile harakati ya kuwa yeye ndiye anasaidia zaidi, anapewa uhaki wa kuridhi mali ili anaridhi mali kwingine anaridhi kwa mumewe, na anaridhi kwa babaye. Kwa hivyo kama Katiba ya Kenya ingezungumza na iwe explicit, ingekuwa ni vizuri sana kwamba itwambie ni yupi ambaye ataridhi mali, ili to avoid ile mtu anatoka kwa bwana yake, anakuja ku-claim mali kwao.

Jambo la pili ni kuhusu Chapter 5 ya Constitution, ambaye it talks about the Bill of Rights. Hapo ndiyo kuna, nafikiri kama si mimi niliona vibaya kwenye Katiba, kuna Rights, Article 41, kuna jambo ambalo lilikosekana hapo. The rights of a person who is tuseme in custody or yule ambaye amekuwa apprehended by the Police. Kitambo nadhani kwa Constitution ya Kenya kulikuwa na uhaki wa kupewa ile simu moja na Police ili uwasiliane na watu ambao wanaweza kuja ama unaweza taka wajue you are in custody. I think when it comes to that Article, maybe in the Constitution, inastahili iingizwe na isisitizwe kamili ndiyo kila Mkenya ajue akiwekwa kwenye koro koro za Police watu wake watajua namna gani. Kwa hivyo Madam Commissioner, I think hizo ndizo zilikuwa point zangu.

Oh yes, na ya tatu ya mwisho ni kuhusu pesa za Kenya. Pesa za Kenya bila shaka huwa zinatumia pesa nyingi sana or a lot of foreign exchange is spent when we are printing this money. Jambo lile ambalo ningependelea kama mwana Kenya ndiyo hizi

pesa tutumie kwa njia nygine, ni kama ingewezekana tuweke kama nchi zile zingine, picha ya aidha Rais ambaye alituleta kwenye uhuru the independence President, ama pili tuweke picha ya kitu ambacho we admire or we treasure in Kenya kama a mountain, a river or something of that nature. Kwa hivyo hii ku-print every now and again nafikiri hiyo si mzuri kwa uchumi wa Kenya. Thank you very much.

**Ezekiel Mutuku:** Asante sana Madam Commissioner, na wananchi wenzangu. Kwa jina naitwa Ezekiel Mutuku. Ningetaka kwanza kuwashukuru nyinyi kwa kutupatia nafasi hii ya kutoa maoni Kwasababu inatupatia kujisikia kama sisi ndio wenye hii nchi, na ndio stakeholders wale wakubwa wa nchi hii. Katika Katiba hii yenu, nime-inenda through and I have supported it, na kwa maoni yangu nimeona kila kitu ifanyike chini ya Katiba hii mpya. Lakini ningetaka kuzungumzia mambo matatu ama mawili, na ya kwanza ni equality. Unajua Kenya hii yetu tumeongozwa na Mungu tangu mwanzo. Mungu amekuwa ndiye mlinzi wetu, na ndiye ametuongoza tangu tupate uhuru. Wakati aliumba mtu mwanadamu, aliumba mwanamke akiwa chini ya mwanamume. Mambo mengine ambayo imewekwa tuwe equal na wanawake, imepita hata kiasi ya Mungu. Hiyo tumeiona tangu wanawake wetu walipoenda Beijing, waliporudi tumeona already so many divorces. So, I am thinking that we should not be equal with our women.

Secondly, I want to talk about money, Kwasababu pesa ya Kenya kuna watu wanaumia na wengine wanafaidika nayo. For example, you find that in the Commissions we have, in a Commission whereby the Commissioner is appointed by the President himself, you have the money being distributed unequally. Unapata watu wale wa juu sana kama umeongezwa 200% wanaongezwa, na watu wale wa chini hawafikiriwi. Kwa hivyo mimi ningesema nyinyi kama Commissioners, you find a method by which wale watu wa chini in every department of this country be considered. Utapata kwamba kama sasa walimu wamegoma, na watu wengine wamegoma, lakini kuna mahali pengine watu hawawezi goma because of the pressure from above, and the people who are in the basis of the departments are not being considered na hawawezi goma Kwasababu watu wanakuwa considered hapa Kwasababu wamegoma. Kwa hivyo hawa watu wanaendelea na kuumia sana na hata wanashanga. They do not know what to do, because maybe their Commissioner was appointed by the President, or maybe he is under the Government or something like that. Kwa hivyo mimi naonelea ni nyinyi mtajua vile mtafanya mteteo hawa watu, na ndio wengi. Utapata mtu analipwa one million in a department, na mtu mwingine in the same department analipwa five thousand which is very much unfair. Hiyo mimi ndiyo nilikuwa nataka kuteta tu. Asante sana.

**Andrew Mutunga:** Nashukuru kwa Commissioner Madam, na washiriki wale wengine. Asante sana kwa kunipa hii nafasi. Nataka kugusia kidogo. Jina langu naitwa Andrew Mutunga mbishara hapa Matuu. Nataka kugusia kidogo mambo ya wanaume na wanawake. Nimesikia ya kwamba kuna equality ama usawa wa mwanamke na mwanamume. Ni lazima kwanza sisi sote mwanamume na mwanamke ukisema hivyo ufikirie kwanza tangu mwanzoni kama hiyo imekuwa na kama ilikuwa, uweke right, kama hakuna ufikirie kwanza. Wakati tunaenda kuchimba chini, unasikia mwanaume anaenda kuchimba level ama mtaro. Nitachukua bibi yangu nimuambie chukuwa jembe na mimi jembe tuende kazi? Hiyo ni kitu ya kufikiria sana.

Ile ingine, wakati pametokea jambo fulani muhimu, unasikia nakimbilia mume wangu. Kwanini yeye haiingii hapo? Kwasababu hawezi. Kuna mambo mazito mazito yanafanywa na wanaume, ndio ninasema kwanza tufikirie. Kama Mungu kwanza amesema mwaume kwanza mwanamke nyumma kidogo. Zile law zote zinatengenezwa, zinatengenezwa kutoka kwa amri kumi za Mungu. Inaonekana ni kama tumevunja hizo amri kumi za Mungu. Sitasema ni ubaya kuweka wanawake sawa na wanaume, lakini kwa mambo fulani. Kama umezaa watoto wawili, kwa mfano umezaa mtoto wa mwanaume na mwanamke na huyo huwa mali yako wanagawanywa katikati na huyu mwanamke atakuja aolewe, huko ameenda anaridhi, ako na mali yake. Kama anataka ku-divorce huko atachukuwa nusu ya mali ya mume wake, na hapa atakuja kuongezewa. Hapo ni usawa kweli? Lazima hapo tufikirie Kwasababu huyu ataenda apate mali ingine huko ameenda kuolewa, na hapa umemwacha umemugawia sasa hiyo itakuwa namna gani? Lazima kwanza tuangalie. Lakini kama hajaolewa mimi napendekeza ya kwamba tugawiwe pamoja tuaagiwe sawa sawa.

Kile kingine naweza kusema, tumeona ya kwamba kati ya Katiba yetu inasema ya kwamba hata mtoto akiwa amezaliwa nje ya ndoa, wewe ulee nisawa. Lakini na-uliza, itategemea. Ni wangu ama ni wa nani, na huyo amekuja kunizalia mtoto hapo aniweke mzigo, na yeye ataenda wapi? Lazima tufikirie kwanza wakati tunasema maneno na wakati tunasema hiyo ni sawa. Haya, mimi nauliza hiyo Katiba yetu tunatengeneza, hiyo Katiba, na sio mchezo. Kama mnaona vile nchi inakimbia na watu kama vile wamejaa, hakuna nafasi na hakuna kazi na hakuna mali. Lazima tuwe tunaangalia matumizi na kila kitu, ujue wewe uko na uwezo wa namna gani na ni lazima uwe unajua Kwasababu mimi niko na uwezo wa kulea watoto wawili sita ongezea mwingine, na hiyo utakubaliana na bibi yako. Afikiria aone hapana mimi siwezi kukaa na watoto wawili Kwasababu fulani ako na watoto watatu naona anakaa vizuri, akuepuke akimbie aende achukue mwingine, na Katiba inasema mimi nilee hawa watoto. Kweli tutakubaliana? Sioni kama tutakubaliana na ndiyo tunazuia pasiwe na utatanishi.

Tunaona kati ya society kuna sheria za ki-society kama mimi Mkamba. Mwanamke hawezi kuwa juu ya mwanaume, mwanamume hawezi kuwa sawa na mwanamke. Lazima uwe unaongoza boma yako na kama tuko sawa na tumependekeza tuwe sawa, inaonekana mambo yote yakija tugawane hata kama ni nini. Ndiyo nasema Kwasababu watoto wamepewa usawa na mwanamke amepewa usawa na mwanaume, akitoka kwao, inaonekana ni lazima akuje na ile uridhi yake huko na mimi ile yangu huko ndiyo tukuje tuweke pamoja. Tukikosana achukue nusu yake, na mimi nibaki na nusu yangu. Hapo tumetoka.

Kile kingine naweza kusema, ya mwisho, sijui serikali yetu italinda mali yetu namna gani, Kwasababu utaona tumefunguliwa kwenda kuweka citizen huko nje. Mimi nitakuja nichukue mali yangu ni weke huko, na mimi nitakuja kuharibu hapa. Nikiharibu na niki beba mali ya Kenya niende nikaweke huko na nimepata u-citizen mwingine huko, hapa kwetu tutabaki na nini? Situtaenda karibu sote, na (inaudible) ambao hawawezi kutoka. Unaona? Ndiyo nasema kama ingewezekana Kenya ingelinda kila mtu aweke mali yake hapa na kama ako na citizenship awe anaangaliwa huko nje anaweka rasilimali kiasi gani. Sio atoe pengine yote Kwasababu ya kuona hapa, atakuja kuharibu hapa halafu akimbilie huko. Ndiyo tunasema, kama inawezekana, awe akiwa anatoroka aangaliwe ana kimbia na rasilimali ya Kenya namna gani. Thank you.

**Com. Ali:** Asante. Do you have a question? I can only allow you to ask a question or a comment on the Draft Bill.

**John Kimwea:** Jina naitwa John Mutua Kimwea, na mimi ni Chairman wa Yatta Constituency Committee. Nimechunguza kwa makini yale ambayo yako katika Draft. Nimeona ni mengi ambayo tuliyatoa kwa Commission, na wameyaandika kama vile tulivyo wapa. Ni kweli sisi sote tunaunga mkono Katiba mpya na ni kazi ngumu. Wale Commissioners wamefanya kazi ngumu, na wote ambao wamehusikana na kutengeneza hii Draft, ni sharti tuwashukuru na pia tuombe hii Draft ikubaliwe. Tungaliuliza hata na mtukufu Rais wetu asije akavunja Bunge lililoko sasa kabla wao hawajaichunguza na kuipitisha. Ni maoni yetu tukifikia uchaguzi mkuu ujao tuchague viongozi wetu kufuatia Katiba tuliyotengeneza, ambao sasa ndiyo hii tunaita Katiba Draft. Asante.

**Com. Ali:** Asante. Tafadhali jilandikishe pale. Asanteni kwa maswali yenu, nitajaribu kuyajibu niwezavyo. Nadhania Mheshimiwa ambaye alizungumza hapa mengi ambayo aliyasema yalikuwa si maswali na sina haja ya kuyarudia wala kuyajibu, isipokuwa hili Article 44 kuhusu freedom of worship, na jambo hili likazungumziwa na swali kuulizwa na Deacon ambaye amezungumza. Nadhania hii Article 44 kwa hakika it is a very wide Article na vile walivyo sema ni ukweli. Inaweza kutumika kwa njia ambazo pengine hazifai, na vile ningeweza kusema ni kwamba ni kitu ambacho mngekiangalia na kuona jini ambavyo tunaweza kuweka vikwazo ama vipimo vya kuabudu, na mkawatumma District representatives ambao watakuja katika kikao cha kitaifa au pia Mbunge wenu kuja na maoni ambayo mnadhania yatatuwezesha kuwa na uhuru wa kuabudu unaofaa.

Bwana Samson Muya aliuliza kuhusu mawakili na kama tuliwaandikia na kuwapatia mawakili masharti ya jinsi watakavyo endesha kesi na zisiwe ndefu. Kwanza kabisa ningependa kumwambia Bwana Muya kwamba kuna sheria ambayo inawakagua na kuhakikisha kwamba mawakili wanafanya kazi yao kwa njia iliyobora. Isitoshe, tukaongezea Katiba maneno ambayo tumeandika kwa Katiba ili kusisitiza umuhimu wa shughuli za mawakili. Hatukuweza kuandika kila kitu, kwa mfano kama kesi isichukue muda mrefu ama mfupi Kwasababu muda wa kesi unategemea mambo mengi sio wakili peke yake. Inategemea washtaka, inategemea mahakama, inategemea mtetezi wa kesi ikiwa ni kesi ambayo ina-Polisi. Kwa hivyo hatungeweza kuwaandika jambo hilo kwa Katiba. Lakini ukiangalia katika Article ya 212, 1(C) tumependekeza kwamba mawakili wawe waadilifu na wafanye kazi yao kwa uwaminifu. Katika Article 67, tumependekeza jinsi kila mwananchi ataweza kufanyiwa kesi yake na mahakama kwa haraka iwezekanavyo. Uliuliza kwa nini hatukupendekeza adhabu kwa mawakili, sheria ambayo inawaangalia shughuli zao imependekeza jinsi ambavyo wakili anaweza kuwadhibiwa na hata kunyanganywa licence, kwa hivyo hilo ni jambo ambalo halifai kuwa katika Katiba, lakini sheria na sheria hiyo iko na ikiwa ina hitilafu, italazimika kubadilishwa ili kulingana na Katiba.

Colonel Mativo akapendekeza kwamba watu waandikwe in accordance with quota system. Tulipokuwa tunachukua maoni watu wengi walikataa maneno ya quota system na ndiyo maana hatukuyaandika katika Katiba hii yetu ya leo. Alisema kwamba hatukutaja National Security Intelligence, kweli hatukutaja kwa kirefu, lakini tumependekeza kwamba mkuu wa kikosi hicho akae katika National Security Council na pengine hili ni jambo, ikiwa ni la muhimu mnaweza kuwatuma representatives wenu wajee ili National Security Intelligence pengine maneno yao yaandikwe kwa kirefu. Akapendekeza pia kwamba Chief of



General Staff na wasimamizi watatu, Commanders of the Forces wateuliwe kwa kupitia Parliament, hilo pia ni jambo muhimu na pengine ingeangaliwa katika National Conference, na akapendekeza kwamba pengine tunge fafanua zaidi wazee ni akina nani, hilo pia ni jambo ambalo pengine lingependekeza. Amependekeza Armed Forces day, hatukulifikiria Kwasababu hakuna aliyependekeza, mimi nimesikia kwa mara ya kwanza leo, na pia wa-Kenya waliteta kwamba tuna siku nyingi za holiday ambazo hazifai. Kwa hivyo sijui kama hilo ni jambo ambalo lingependekeza watu wengi, lakini likiwa na muhimu linaweza kuangaliwa katika wakati wa kikao hicho cha kitaifa ikiwa mtapendekeza kupitia waakilishi wenu.

Bwana Julius Kilonzo anauliza kwa nini hatukuwangalia sheria za kitamaduni. Ningewaomba msome Chapter ya pili Article ya tano, tumeweka traditional laws kama sheria ambazo zitatumika katika nchi yetu kwa hivyo tumetambua na kukumbuka vile mlitueleza. Bwana Benjamin alizungumzia Hero's Day na Katiba Day akasema hayo yote yanafaa na akawa hakufurahia kuwa tumeondoa hukumu ya kifo. Sasa, jambo ambalo lilitutaliza kama Tume ni kwamba unasema kuna haki ya maisha, upande mwingine unasema maliza maisha ya mtu lakini jambo ulilosema pengine utawatuma waakilishi wa sehemu hii wailete katika National Conference tuone vile ma-delegates watajadiliana, tuone mawazo ya watu wengi. Sisi tulipochukuwa maoni tulikuwa watu ishirini na tisa sasa tutakuwa watu mia sita ishirini na tisa, pengine tutaweza kufikiria zaidi na kuona kama kunahaja ya kuweka hiyo hukumu ya kifo. Kwa wakati huu tumependekeza watu wote ambao wangehukumia kifo wapewe hukumu ya maisha, wafungwe jela na wasitoke wakae kule mpaka watakapo fariki. Pia, hakufurahia... (end of tape).

Hicho tulipewa na wananchi, hatukukiweka Kwasababu nchi zingine zimeweka ama tulipenda sisi lakini hata ukiangalia maoni tuliyoyapewa na watu wa sehemu hii yenu, mlituambia tuweke kiwango cha umri wa Rais na tukatii amri lakini ikiwa mmebadilisha nia, mambo hayo yanaweza kubadilishwa kwa National Conference. Pengine sasa mmeona hilo sio jambo muhimu. Pia, ningependa kukueleza hivi, kwamba hatukuweka umri huo Kwasababu tulitaka kuwafungia watu wowote. Tulifikiria sana na ukiangalia schedule ya saba 3, ( v ) tumependekeza hivi ili uhakikishe kwamba hatukutumika na yeyote ule. Katika elections, eighth schedule section three sub section five, tulipendekeza hivi, subject to clause 4, any person who would otherwise have qualified to stand for elections but for the provisions of this Constitution is eligible to stand as a candidate in the first elections held under this Constitution. Tunamaanisha kwamba mtu yeyote ambaye anataka kusimama kupigania kiti cha u-Rais na angekuwa hana kikwazo katika Katiba ya wakati huu ataweza kusimama, Kwasababu tunajua kuna viongozi kama wawili au watatu ambao wamepitisha umri huu na wangetaka kugombania kiti cha u-Rais. Kwa hivyo tukahakikisha ya kwamba wasikatazwe ili msitulaumu na kusema tumewafungia nje, lakini baada ya elections hizi ikiwa mambo haya yatakubaliwa katika National Conference, tumependekeza kama tulivyoambiwa, mtu yeyote atakayetaka kusimamia kiti cha u-Rais awe chini ya miaka sabini.

Kwa hivyo, ninataka kukuhakikishia kwamba vijana hawakupenya. Ni mambo mliyotwambia na tukahakikisha kwamba hatukuwakosea wazee kwa kuweka kifungo hicho ambacho wengine wanatulaumu na wanasema tumetumiwa na hawa wazee. So, it depends on how you want to look at it, lakini tumehakikisha vijana na wazee wataweza kupigania kwa wakati huu. Pia jambo ambalo umesema, kuna watu wengi ambao ni zaidi ya umri huo na wametawala kwa njia iliyobora, kuna ukweli katika

mambo hayo lakini nyinyi wenyewe mlituambia pengine Kwasababu mlikuwa mnafikiria kuhusu Rais Moi mkatuambia sasa lazima wazee waondolewe. Lakini kama mmebadilika, we still have time at the National Conference, tunaweza kubadilisha na kuhakikisha kwamba age limit haipo katika mambo hayo.

Village Government, tumeulizwa nani atakaye kuwa Chairman, tumewaachia watu wa kijiji kujichagulia wenyewe, hatukutaka kujihusisha sana na utawala wa kijiji ambapo kutakuwa na wazee ambao watakuwa na hekima nyingi na wataweza kutatua shida na kujua nani atakaye simama. Local Government appears to be removed, yes we removed it Kwasababu tuliambiwa na wananchi tena kwamba kuna-duplication ya shughuli zinazofanywa na Local Government and Local Administration. Sasa tumezitoa zote mbili na kupendekeza tuwe na Local Council katika kata ama location na District Council katika District na Provincial Council katika Province, na tukaeleza shughuli ambazo watazifanya ambazo zilikuwa zinafanywa na administration, au upande mwingine both administration and local authorities na kukawa na duplication of duties.

Kuhusu ukasema Chapter 12, kuhusu environment, mambo ya maji, changarawe na natural resources. Section 239 nafikiri imeangalia mambo haya, tumependekeza pia kuwekwe kamati itakayo chunguza mambo haya zaidi Kwasababu hatukuwa na wakati wa kuiangalia kwa undani. Kuhusu maji ukiangalia Chapter ya tano tumegusia kuhusu shughuli za maji kama haki ya kimsingi na vile kila mwananchi ni lazima aweze kupata maji yaliyosafi na ya kutosha kupitia juhudi za serikali. Ukazungumuza kuhusu PTA and BOG in schools, mambo haya kwa hakika si ya Kikatiba ni mambo ambayo yanatekelezwa katika educational Act, na policy za serikali au misimamo na mielekeo inatolewa na serikali na hatukuweza kuyaweka hapa, lakini katika report ambazo tulipata katika constituency tumeandika kwamba wananchi walitaka kuona mambo haya yafanywe, kwa hivyo yanaweza kutekelezwa katika Education Act ama misimamo na mielekeo tofauti ya kiserikali, hatukuweza, Kwasababu Katiba haiwezi kuwandika kila kitu ni muelekeo tu wa utawala.

Bwana Issac, namuona hayuko hapa, na anashida kubwa sana na ameweza kutupatia msimamo wa Bibilia lakini ningesema huo ni msimamo wa Bibilia anayoelewa yeye. Mimi sielewi Bibilia sana mimi ni Mu-islam lakini nakumbuka kulisimama watu ambao wanaelewa Bibilia kwa undani ambao ni makasisi na wakatuhimiza tuweke usawa katika vitu ambavyo ni muhimu katika maisha na wao walivyotueleza kwamba Bibilia haijasema kwamba mwamamke ni duni dhidi ya mwanamume. Kwa hivyo moja nitajibu swali lake pamoja na watu wote ambao walikuwa na wasiwasi na jambo hili na niwaambie mkiangalia Section 35, 1 and 2, hatujasema wala hatujapendekeza kwamba wanawake na wanaume wabadilishe sehemu yao katika jamii. We have not recommended exchange of roles of men and women. Kijana aliyekuwa hapa ambaye anasema nikiwa na chimba ni mimi nitaambiwa nikachimba kama mwanamke, je ukiambiwa uzae, utazaa? Huwezi. We have not advocated for change of roles.

Tumesema wanawake wapewe heshima na sehemu iliyo sawa katika maendeleo ya nchi yetu, na ndiyo maana kila nyumba ina baba na mama Kwasababu baba hawezi kuzaa na kulea, si niukweli? Mpaka atafute mama. Tunasema hakuna taifa litaloendeshwa na wanaume bila wanawake. Tumependekeza wapewe nafasi hatukusema wapewe usawa katika nyumba, no, wapewe nafasi, equal opportunities. Nafasi za sawa katika siasa, katika uchumi na katika maendeleo ya jamii. Sijui hapo kama



kunatakwishi. Ungetaka mtoto wako wa kike ukimsomesha afike university abaki akipika muthokoi sio? Na asipate nafasi ya uchumi, asipewe nafasi ya kazi. Tunasema wapewe nafasi sawa katika juhudi na mambo yatakayo tuendeleza kitaifa. Pia, tukasema wahesimike wanavyo heshimika wanaume. Pia tukasema wapewe haki ya uridhi, Kwasababu kwa wakati huu, wanawake wengi wananyanyaswa na kuyimwa haki ya uridhi hata pale wametoa jasho.

Ukiangalia ukweli wa maneno kwa wakati huu na maisha yalivyo, akina mama pia wanachangia uchumi wa nchi. Mtachuma na bwana wako, lakini akikupiga teke anakwambia mali ni yangu. Kwa hivyo tumesema ikiwa kuna uridhi pahali popote, kwa mfano bwana akifariki na huyu mama amechumma mali na bwanake, asifukuzwe na jamii, lakini apewe haki ya kuridhi. Ukiwa na watoto wawili wakike na wakiume, kwa yule amasema kwamba the Constitution is not explicit, for me it is very clear. Imesema pale kuna uridhi, mwanamke apewe uridhi uliosawa na mwanamume. Kwa hivyo kama ni kwa bwana, kama ni kwa babake apewe. Lakini mkiona jambo hilo ni zito, mtapendekeza mambo ambayo mnaona yatakamilika na yatakuwa sawa kupitia kwa waakilishi wenu. Pia, jambo ambalo tulisema ni kwamba ikiwa kunasheria yeyote ya kitamaduni ama practice yeyote ambayo itaweza kumnyayasa mwanamke, sheria hiyo itupiliwe mbali.

Pia, pengine ningesema kwamba katika National Conference, tutakuwa na waakilishi zaidi ya kumi na sita ambao watatoka katika madhebu tofauti ya kidini, kwa hivyo kama kwa hakika Biblia imesema mwanamke anyimwe haki ninahakika watatuambia siku hiyo, na kuweza kutatua jambo hili Kwasababu sisi pengine hatukuelewa zaidi na pengine Biblia imesema kama mlivyotuambia. Pia, akawa na shida kwamba tumependekeza Locational Government iwe na wanawake wawili, samahani nafikiri haukuelewa. Tumependekeza kwamba kuwe na two representatives. Na Kwasababu kawaida ni kwamba ukipendekeza two representatives wazee watatokeza wazee wawili, ndiyo tukahakisha kwamba mmoja awe ni mama, lakini nikasema sheria haijasema mmoja ni lazima awe baba. We are silent because practice ni kwamba tusiposema mama awe, wazee watatoka na kuwaambia mama warudi jikoni na hatutaki hivyo. Akina mama walisema wangependa kuhusishwa katika utawala wa nchi.

Titus Mwaniki, what happens if the proposals hazitakubaliwa na Rais? Mtaweza kumsikiza au mtafanya vipi? Ningependa kusema katika sheria ambayo inawasilisha kazi hii, Rais hajapewa uwezo wakubadilisha kama mtu binafsi. Sheria imesema kwamba baada ya kuchukua maoni, tutaandika Draft Constitution, itaweza kujadiliwa katika kikao cha kitaifa. Pale watu ambao watakuwa katika kikao cha kitaifa wanaweza kubadilisha na pia itapelekwa Bunge kujadiliwa na pia kama tunavyojua kazi ya Bunge ni kuwalia sheria. Wanaweza wakitaka kubadilisha, lakini tunatarajia kwamba Kwasababu wote wataketi katika kikao cha kitaifa, kwamba mambo haya yakisha kutatuliwa katika kikao cha kitaifa kitakwenda Bunge tu kuidhinishwa na kupitishwa. Kwa hivyo hatujapatiwa ruhusa ya kuzungumza na Rais ama mtu yeyote ambaye ana ukumbwa, ili kugeuza mambo ambayo yametolewa na wananchi. Pia akazungumzia kuhusu kura, na shida ambazo ziko pale. Nafikiria katika Article ambayo tumezungumzia kuhusu mambo ya kura tumewapatia Electoral Commission nguvu ya kuweza kutatua na kuhakikisha kwamba mambo haya hayatendeki na kikawaida Polisi wanaambiwa waweke nidhamu na kuhakikisha kwamba hakuna mambo ambayo ni ya hatari katika kazi zetu za kawaida.

Francis Kyalo, pia alizungumza kuhusu problems of elections na kama tutaweka supervision ya political parties, hii kazi tena imepatiwa Electoral Commission, na ningekuomba usome Article 88 and 85. Akasema kwamba chama kinachotawala kitakuwa kinashinda Kwasababu kiko in charge of elections. Je, vyama tofauti vingeweza kupewa watu wao ambao watasimamia wakati ambapo kura zinahesabiwa? Ninavyoelewa ingawa mimi si mwanasiasa ni kwamba kila chama hupewa nafasi ya kutoa watu watakao kaa sehemu ambazo kura zinahesabiwa, lakini ningependa kukwambia kwamba katika hii Katiba mpya tumependekeza kwamba Tume ya upigaji kura iwe ni huru na inajisimamia bila kujihusisha na siasa za pande zozote, na pia kwamba kura zihesabiwe katika pollings stations na pia tukapendekeza kwamba tuwe na transparent boxes, kwa hivyo mambo hayo yatakuwa yametatuliwa. Pia akauliza je, mtatuhakikishia kwamba kura zitakuwa katika Katiba mpya, siwezi kukuhakikishia kwasababu Tume yetu haina uwezo wa kuhakikisha wala kujihusisha na kura za wakati huu. Nadhania sote tunajua mtu ambaye ana wadhifa wa kuitisha kura na ni Rais. Nadhania yeye peke yake ndiye anaweza kuhakikisha kuona kura inapigwa katika Katiba mpya ama ya zamani.

Elijah akazungumza kuhusu corruption, na anafikiria kwamba hatukutia mkazo katika hili jambo la corruption. Ningependa kukuelezea kwamba jambo hili limezungumziwa. Ukiangalia Article 15, na pia ukiangalia katika values, Article 14C 6, tumepedekeza kwamba serikali iondoe rushwa, na hizi ni katika values ambazo zitatumika katika Katiba na katika mambo yote tutakayo fanya katika shughuli zetu. Ukasema kwamba hatukuweka Anti-Corruption Unit, ndiyo hatukuiweka, Kwasababu mambo haya tumesema yazingatiwe na kila Mkenya, na pia ni jambo ambalo pengine linaweza kuzingatiwa ikiwa ni jambo la muhimu sana katika National Conference Kwasababu hatukudhania tulikuwa na haja ya kuweka Anti-Corruption Unit.

Margaret ali-support equality. Bwana Jackson Mwinga alitaka kujua hawa watakao tawala katika location watafanya kazi kwa muda gani, hatukuandika, na pia Kwasababu ni watu wametumwa kutoka kwa kijiji, ikiwa ni watu hawawezi kufanya kazi, wazee wanaweza kuwaita na kutuma representatives wengine lakini pengine hilo ni jambo ambalo tunaweza kuliangalia katika National Conference ili kuondoa matatizo ya watu ambao wamepewa vyeo na kukaa kule kwa miaka mingi.

Julius Muli, amenistajabisha sana kwa swali lake, sijui kama ako. Julius Muli ako? Kwasababu, Bwana Muli, unasema kwamba hawa watoto ambao kwa Kiswahili wanaitwa wanaharamu, wao huwa wanavunja nyumba. Ni mtoto anavunja nyumba, ama ni wewe ulienda kutafuta huyu mtoto? Kwasababu kama hukumtafuta hangekuja, so I do not know how you are blaming the child. Nimestaajabu sana na swali lako hata ninashindwa kukujibu Kwasababu ikiwa ulienda kutafuta mtoto, sasa unalalamika nini, Kwasababu mtoto huzaliwa kupitia kwa mwanamume na mwanamke si ni ukweli? Ukitoka ukijua uko ndani ya ndoa na unaaenda nje kumtafuta huyu mtoto, kweli tunaweza kumlaumu? Ndiyo maana tunasema ama tunapendekeza kwamba mtoto huyu hana hatia. Alitafutwa na watu wawili ambao ni lazima wa-take responsibility ya kumulea, na kuondoa watoto ambao wako katika streets na ambao wamekosa kulelewa na wazazi ambao wanafanya vitendo ambavyo baadaye hawataki kuviangalia. Kwasababu ikiwa kweli umeoa hutaki kuvunja ndoa yako, ulikuwa hauna shughuli ya kwenda na kutafuta mtoto nje.

Nafikiri that is squarely the responsibility of men and women and not children, ndiyo maana tumesisitiza ni lazima waangaliwe na wazazi wote wawili, iwe ni mwanamke au mwanamume kwenye ndoa na nje ya ndoa. Pia ukasema getting a child out of marriage is serious, yes it is serious business that is why you should take responsibility. Nafikiria kwa Kiingereza tunasema you can not have your cake and eat. If it a serious affair, ukipata mtoto basi unamuangalia. Ukazungumzia inheritance, nafikiri nimejibu lakini nataka tu kukupa jambo moja, kwamba ikiwa tunatoa maoni, it is good to look at reality and be serious, katika jamii, nadhania mtu ambaye hutoka na kuwacha watoto na kuenda kwa club sio mwanamke ni mwanaume. That is the reality, kwa hivyo hata hili neno ambalo unasema sijui kama unaweza kusimama mbele ya umati ya watu mia sita na kuweza kulipendekeza if you are serious. Watu ambao wanawachwa na mzigo wa kulea watoto ni akina mama. That is the reality. Out of 100 women, mmoja ndiye atatoka kwenda kwa club. Kwa hivyo, you may have a point lakini nafikiria ulivyoliweka lile point yako, ni kitu ambacho hauwezi ku-convince mtu yeyote, na sidhani na hatukudhania kama Tume, kwamba mama akipewa mali itakuwa inapotea. Tulifikiria kwamba wakigawanyishiwa, ile mzee angepoteza huko kwa club itabakia na mama na watoto.

Mkazungumuza kuhusu pesa, nafikiri hili ni jambo tuliliweka katika report yetu. Hatukuweza kuliweka katika Katiba, na tunafikiria ni jambo litazingatiwa Kwasababu lilizungumzwa na watu wote. Death penalty, nimelizungumzia na ukataka kujua ni kwanini nchi zingine watu wanaadhibiwa na kupigwa mawe na huku tunaondoa. Hili ni jambo ambalo pengine lingerudiwa katika National Conference, ikiwa ni jambo ambalo lina uzito. David Mativo, freedom of worship, nafikiri nimejibu. Patrick Kyalo, hana shida na equality, lakini anasema mbona mwanamke anachungwa wakati ambapo kuna watoto wa nje, na kwamba kuna wanawake wale wanaweza kudanganya wanaume na kuzaa watoto ovyo ovyo. Is he here Patrick? Yuko? Are you married? Sijui kama kuna mwanamke ambaye anaweza kutaka kupata mtoto ovyo ovyo ili a pin down mwanamume. I think there is much more to giving birth, isn't it? That is why I am saying, let us be serious. There is much more in getting pregnant than just wanting to pin a man down, na hata kama iko, nafikiri those are isolated cases and I do not think we are trying to protect women. We are trying to protect the children who are on the streets, because of irresponsible behaviour by men and women. That was the intention of the Constitution and the intention of the Commission.

I think Ambrose, nimejibu that as far as I am concerned, the Constitution is explicit on who is a woman. You inherit where there is property to be inherited, for me it is very clear. Lakini kama kuna uzito tena kwamba wanawake wanaweza kutajirika kwa kupata mali pande zote, that is an issue that can be discussed at the National Conference kupitia kwa waakilishi wenu ili mambo haya mazito yaangaliwe. Pia ukasema Bill of Rights kwamba tungeangalia haki za watu wanaoshikwa. Section 67 and Section 68 broadly gives the right of arrested persons, but again you gave a point that there should be a right to communicate with the family, that is something that can be taken up either under ordinary law or the Constitution, it is a good point. You spoke about currency, I have already answered that. Ezekiel Mutuku, amesema nimekubaliana na hiyo Katiba yenu. Bwana Mutuku, Katiba si yenu, ni yetu, sisi wote. Nyinyi ndiyo mlituambia tukaandika Katiba na akazungumzia equality, ame zungumzia kuhusu Mungu, God created woman to be under men.

Since you are talking about the Bible I do not have much to say but the little I have heard people say, is that alumbwa kuwa companion ya mwanaume, sio kuwa chini ya mwanaume. That is the way I understand my little knowledge of the Bible, sijui kama ni ukweli ama ni uongo. Ukazungumza about unequal pay na kama tungejaribu kuhakikisha kwamba watu wanalipwa mishahara ambayo inastahili. Ukiangalia Section ambayo inazungumzia Section 55, haki za wafanyikazi, tumependekeza kwamba wafanyikazi wapewe fair remuneration, pesa ambazo zinastahili kwa kazi ambayo mtu anafanya.

There was a young man, I did not get his name, alizungumzia equality, habari ya kuchimba, nataka kumuambia kuchimba hata sio kazi. It is very easy compared with what women go through. Nafikiri wakiambiwa wachimbe watachimba kabisa, ikiwa hakuna wanaume. Pia akasema Mungu alisema mwanaume kwanza halafu mwanamke, mambo hayo I think we will have experts. Kama nimesema kuna ma-Reverend wengi sana watakuja huko zaidi ya kumi, na kuna Sheikhs, watakuja huko wataambia mambo haya kwasababu, nadhania hata wewe pengine sio mtaalamu sana wa Bibilia. Sasa kutakuwa wataalamu wataweza kutuongoza tuone jambo hili liandikwe ili tusiwe tunakosea neno la Mungu. Kikakueleza kwamba Katiba inazungumza kuhusu opportunities, na unafikiria kwamba kukiwa na usawa kutakuwa na divorce nyingi. Nafikiria divorce ziko hata wakati huu ambapo hakuna usawa si ni ukweli? Kwa hivyo, hili jambo sijui kama litakuwa la ukweli ama ni namna gani.

Pia, uliongea kuhusu hawa watoto wa nje, kwamba unauliza nitajuaje huyu mtoto ni wangu ama si wangu. Ningetaka kukujibu mambo mawili, kwanza ukienda huko nje hiyo ni risk unachukuwa kwa hivyo itakuwa ni bora usiende, ukae kule unajua watoto watukuwa ni wako. Pili, kuna utaalumu siku hizi, ikiwa unakataa kuna wataalamu wale wanaweza kutatua na kusema kama wewe ni baba ama si baba, kwa hivyo kuna suluhisho hapo. Pia, unasema mimi naambiwa ni chunge mtoto, je mama anaamibwaje? Sheria ukiangalia Article 37 3(1), inasema baba na mama wawe na jukumu sawa. Kwa hivyo hujaambiwa ukizaa nje wewe umwangelie mtoto na mama asiwe na jukumu, tunapendekeza wazazi wote wawili wawe na jukumu la kulinda mtoto. Pia, ukasema bibi yako ukiwambia azae watoto wawili anaweza kukimbia na kuzaa mtoto nje. Sijui kama, umeoa? Unadhania bibi yako anaweza tu kuzaa ovyo ovyo akuletee mtoto? You know, some of these things are not as easy surely. Bibi atataka kuzaa nini, alete tu mtoto basi aonange watoto watatu? That is not a reality kijana, haifanyiki na pia mnafaa mzungumze, sio wewe unatoa amri usizae. If there is equality, ama uhusiano mwema katika family watu hukaa na wakapanga pamoja si ndiyo? Yes, lakini si dhani, I am a woman, I do not think I can get a child for the sake of getting a child. There is more to it. Kuzaa sio rahisi, pengine inaonekana ni rahisi, lakini zungumza na mama nyumbani atakuwambia it is a tough job. Nadhania kufika hapo nimemaliza maswali na nimewashukuru. (interjection) Yes Please.

**Speaker: (interjection):** Sorry for interrupting. The question about  
(inaudible).

**Com. Ali:** You know, you can not be a Governor and then you are not paid. It is obvious. Si Provincial Administration wanalipwa? Si Councilors wanalipwa? Si chief analipwa? I think it goes without saying, that if you are involved in Governance

you must be paid. You know there are certain things we can not put in the Constitution, but I am a hundred percent sure they are empl oyees and they have to be paid. Thank you very much, tumewashukuru kwa kujitokeza kwa wingi na kuweza kufanya mkutano huu ukawa mkutano mzuri na wa manufaa na nitawarudisha kwa Rose kufunga mkutano.

**Rose Kimeu:** Asante sana Madam Commissioner kwa mawaidha yako. Tumesikiza, tumekuelewa, na tunatummaini kwamba watu wa Yatta watakapoenda kutumma Mbunge wao ama mmoja wa wale watatu wawaakilishi wa Machakos District kwa Constitutional Conference, watakuwa wanatuma watu wakielewa ni kitu gani yenyewe wangependa iwekwe katika Katiba mpya. Kwa hivyo asante sana Commissioner, na wacha nichukue nafasi hii niwaulize wananchi wa Yatta kama kuna mmoja wetu mwenye anaweza kutufungia mkutano kwa maombi. Tafadhali jitokeze ukaweze kutufungie mkutano.

Commissioner amenikumbusha kwamba niwaeleze hawa watu watatu representatives wa District kwa National Constitutional Conference ni akina nani, na pengine ningechukua nafasi hii niseme kwamba tuko na wao, watu watatu walichaguliwa na County Council ya Machakos kwenda kwa Constitutional Conference, na mmoja wao ni Councillor wa Wamunyu, mtu anaitwa Councillor Stepstone Ngalatu Musao, yeye ni Councillor wa Wamunyu Location, na kuna mwingine anatoka Kathiani Division, jamaa anaitwa Stenlords Kasoka, ni wa Kathiani Kaiwa Location, na kuna mama ambaye ni lawyer by profession, anaitwa Victoria Mutheu Musioka. Victoria pia anatoka Mwala Constituency lakini katika Locational ya Viulia. Kwa hivyo, hawa ndiyo watatu wenye waliweza kuchaguliwa.

Hatukubahatika kupata mmoja kutoka upande huu, lakini hawa ni watu wako accessible. Ni watu wale for some time sasa watakuwa wakitembelea Constituencies zingine pia waweze kujua ni kitu gani kinatokezea. Kwa mfano, walikuwa Kangundo kwa ile miktano tulikuwa nayo Kangundo, na ile ilikuwa Machakos pia walikuwa. Walikuwa ya Mwala lakini kwa bahati mbaya pengine hawakuweza kufika kwa huu mkutano wa leo. Pia, Wabunge wote ni members kwa hiyo Constitution Conference, kwa hivyo unaweza kutuma Mbunge wako. Mheshimwa Wambua will be a member in that Conference, so that may be the formation I can give for now. Ni mtu mgani ataweza kutuomba sasa? Kunaye? Karibu.

**Titus Mwaniki:** Na tuombe. Baba, katika jina la Yesu, tunakushukuru kwa kuwa umetuweka ka muda huo wote. Baba yote tuliyoyazungumzia ni ya manufaa kwa wananchi wa Kenya kwa jumla. Baba, tunakuomba kwa hivi sasa hivyo tumemaliza mkutano na Baba tunakuomba uweze kuwa nasi kutoka hapa wale tunaenda na magari Baba uweze ukatuongoza. Baba, hata tunaomba kwa amani katika nchi yetu Baba, hata Baba tunaomba Commissioner na wale wengine wamekuja nao pamoja uweze kuwaongoza kwa safari yao hadi kulewanapoelekea. Baba, kuwa nasi hadi kutoka sasa hadi mwisho. Katika jina la Yesu Kristu tumeomba. Amen.

Meeting ended at 2.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**